SUPA JACKPOT
TZS. 1,027,393,141
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 9

## MCHUNGAJI jela miaka 30 kwa kosa la ubakaji


NI ZAMU YA MGOMBEA HURU
LHRC wakumbushia hukumu kesi ya Mtikila, watamani serikali imruhusu

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Uchaguzi Angola: UNITA yaanguka kishujaa kwa MPLA, ikisomba 62% kura jijini Luanda

FAHAMU CHIMBUKO LA UWANJA JOHN MWAKANGALE

Jina la penye maonyesho kilimo kumuenzi mkongwe wa Mbeya

- Kipenzi mkoa, Nyerere aliyemkaribisha Mandela 1962
- RC mstaafu Paul Kimiti asimulia walivyolikokotoa jina

UKURASA 11

# Nipashe

Jumatano Agosti 31, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581054

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Samia aiwakia polisi

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) mstaafu Omari Mahita, baada ya kufungua kikao kazi cha maofisa wakuu waandamizi wa Makao Makuu ya Polisi na Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Vikosi katika Chuo cha Polisi (CCP), mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: IKULU**



## Mbunge abanwa huduma mama na mtoto chini ya mti

UKURASA 2

Baadhi ya kinamama wa Mtaa wa Saranga, wilayani Ubungo, mkoani Dar es Salaam, wakipata huduma ya kliniki ya watoto chini ya mti wa mkwaju hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wahalifu wavamia mtaa, wapora fedha na kujeruhi

UKURASA 3



Mmoja wa majeruhi Abdul Salum Maketa.

UKURASA WA 4

### AFARIKI DUNIA AKIJARIBU KUJIOKOA NA MOTO

REHEMA Chande (70), mkazi wa Mji Mkongwe mjini Unguja, amefariki dunia baada ya kujaribu...

UKURASA WA 3

### WADAU WATAKA MABADILIKO YA SHERIA, KATIBA MPYA

ZIKIWA zimebaki siku 16 kuelekea maadhimisho ya Siku ya Demokrasia Duniani, wadau wa siasa na...

MICHEZO YANGA YAITOLEA MACHO AZAM UK.24

MAONI, KATUNI UK.6




Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillus Wambura (kulia), akizungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wa pili kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo, katika kikao kazi cha maofisa waandamizi wa Jeshi la Polisi kilichofanyika katika Chuo Cha Polisi (CCP) Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. Benki ya NMB ni mdhamini mkuu wa kikao hicho. Kushoto ni Mkuu wa kitengo cha Biashara za Serikali wa benki hiyo, Vicky Bishubo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia aiwakia polisi

**Na Waandishi Wetu,**
MOSHI

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema ana taarifa za baadhi ya viongozi wa Jeshi la Polisi nchini kutumia ndivyo sivyo mafuta ya magari yaliyohifadhiwa kwenye bohari kwa kuyaweka kwenye magari yao ya biashara.

Alisema ana ushahidi kwamba wengi wa maofisa wanachukua mafuta hayo na kuweka katika vyombo vyao vya usafiri yakiwamo mabasi madogo ya abiria maarufu kama Hiace.

Rais Samia alizungumza hayo jana katika Shule ya Polisi Moshi (TPS), wakati alipokwenda kufungua kikao kazi cha Maofisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi Makao Makuu, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Vikosi.

"Nimpongeze IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini), kwa kusema fedha ya mafuta inashuka mpaka kwenye ngazi za wilaya. Nina taarifa kwamba askari hawapati mafuta kwa ajili ya kwenda kufanya kazi zao na badala yake baadhi ya viongozi wanachukua mafuta kwenye bohari, kwa ajili ya kuweka kwenye magari yao ya biashara.

Wakuu, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Vikosi.

Alisema fedha zinazotumika kununua mafuta hayo ni za serikali, mafuta yanapaswa kutumika kuwatumikia wananchi. "IGP nina ushahidi wengi wa maofisa wetu wanachukua mafuta na kuweka katika vyombo vyao vya usafiri zikiwamo Hiace."

Alisema hawatavumiliwa kwasababu ni kosa na kumuagiza IGP kuhakikisha mafuta hayo yanakwenda kwa askari ili waweze kuboresha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

### MFUKO WA KUZIKANA

Akionyesha kukerwa na matumizi mabaya ya fedha za Mfuko wa kufa na kuzikana, Rais Samia, alisema yapo matumizi mabaya ya fedha za askari kwenye mfuko huo kwa kuwa baadhi ya askari wanapofiwa hawapewi, licha ya michango kufanyika.

"Huu mfuko ni nguvu za askari, mfuko wa kufa na kuzikana. Fedha zinakaa kwenye akaunti za jeshi, lakini matumizi yanapofanywa askari hawana taarifa. Ripoti za fedha hakuna, nilikuwa naongea na CAG hapa (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali), akanambia ameombwa kufanya ukaguzi maalumu, maana ushirikiano kwa wale wanaofiwa hakuna.

"Kama Mfuko ni wa Kufa na Kuzikana, basi watu wapewe wanapofiwa na hiyo fedha itoke, lakini unakuta fedha zinatoka na askari wanafiwa na hawafaidiki na wanaofaidika ni wachache. Lakini ukienda kutizama fedha zilizochangwa hazipo zimetumikaje haieleweki."

### JESHI NA WAHISANI

Rais Samia, amelionya Jeshi hilo kutumia wahisani wanapofanya vikao kazi na kulitaka kujipanga.

Alisema kuwatumia wadhamini katika kuwezesha kuendesha vikao hivyo, kutawafanya washindwe kuwaadhibu wanapofanya makosa.

Alikumbusha kuwa kikao kilichofanyika jana kimedhaminiwa na taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za serikali ambazo nazo zina binadamu na wanaweza kufanya makosa na wakashindwa kuwashughulikia.

"Leo tumekuja tuna wadhamini kama watano, sita wametudhamini, lakini kama Jeshi la Polisi kikao kama hiki, tunatakiwa tukifanye wenyewe, tujipange wenyewe."

### MAADILI

Kuhusu kuporomoka kwa maadili katika Jeshi la Polisi, Rais Samia, alisema kumesababishwa na kukosekana kwa mafunzo.

"Kwa sasa tumewekeza nguvu kubwa katika kuhakikisha mafunzo hayo yanapatikana.

"Wanaofanya vibaya ni lazima warudishwe, Jeshi lisionekane tu ni kichaka cha kupeleka watu kuliharibu. Tumetoa bilioni 11 ili kuhakikisha vijana wanapewa mafunzo, pamoja na hilo itazameni mitaala kama ni ile ile toka enzi na enzi? Mnapaswa kuwa na mitaala inayoendana na TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) ili kuwasaidia askari kukabiliana na mabadiliko ya kimfumo duniani."

### AKERWA SARE KUUZWA

Alionesha kukerwa sare za polisi kuuzwa katika majeshi mengine kama Zimamoto na Ukoaji.

"Katika kipindi cha awamu ya nne na tano, Jeshi la Polisi lilipata sare nyingi sana, ambapo tulitegemea kukaa miaka mingi, lakini katika kipindi cha awamu ya tano kilio kimeanza upya, hakuna sare.

"Nimejiuliza na kufanya uchunguzi na kubaini zipo ambazo zinauzwa kwa Zimamoto, Blue zinauzwa kwenye maeneo mbalimbali madukani. Zilizoshindikana ni hizi za kaki, kwa kuwa zikiuzwa zitajulikana.

"Kofia mna-share (shirikiana) na Uhamiaji ni kiasi cha kubadilisha nembo tu. Swali rahisi, Jeshi la Polisi, kazi yenu kuagiza na kuuza bidhaa au ni kulinda raia na mali zao? Na kama mnauza fungueni kampuni.

"Kama mnafanya biashara mtuambie, sio kufanya vificho vificho, IGP kasimamie hilo, kama ni biashara fanyeni kwa kueleweka."

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha (Moshi).**

## Mbunge abanwa huduma mama na mtoto kutolewa chini ya mti

**Na Beatrice Moses**

WAKAZI wa Mtaa wa Saranga katika Wilaya ya Ubungo, wamembana Mbunge wa Kibamba, Issa Mtemvu, wakimtaka ashiriki kuondoa kero na fedheha wanayoipata wajawazito kwenye huduma ya mama na mtoto inayotolewa kwenye ofisi ya serikali ya mtaa na chini ya mti wa mkwaju.

Hayo yalijiri mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye mkutano uliofanyika katika mtaa huo uliowakutanisha wakazi wa eneo hilo na mbunge aliyeambatana na Diwani wa Saranga, Edward Laizer.

Mmoja wa wakazi hao, Daria Mbwewe, alimweleza mbunge huyo huku akimwonyesha kamba iliyofungwa kwenye mkwaju inayotumika kuning'iniza watoto kuwapima uzito.

Pia alimtaka aone na kitanda kilichowekwa kwenye ofisi ya mwenyekiti wa serikali ya mtaa ambacho hutumika kupima wajawazito.

"Uchungu wa mwana aujuaye mzazi. Sisi kinamama ni wazazi, tunapata shida wakati wa ujauzito hata baada ya kujifungia. Pia watoto wetu nao wanahudumiwa kwenye mazingira magumu. Mbunge naomba uone watoto wetu wanavyohudumiwa kwenye mti pia uangalie na kitanda wanachohudumiwa wajawazito," alisema huku akishangiliwa na wenzake.

Mkazi mwingine, Joseph William, alitaka kujua ofisi ya mbunge inachangia nini kwa kuwa wananchi wameshachangishwa fedha na ujenzi umeanza lakini bado kuna mahitaji mengi ili zahanati ikamilike.

Kutokana na kibano hicho, Mtemvu aliahidi kuwa mfuko wa jimbo utachangia Sh. milioni 15 kwenye ujenzi huo lakini hakubainisha ni lini fedha hizo zitatolewa.

"Nitumie nafasi hii kuwasisitiza kushiriki kikamilifu kwenye Sensa ya Watu na Makazi kwa wale ambao bado hawajahesabiwa. Hii itatusaidia katika mipango ya bajeti na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo huduma za afya baada ya kujua idadi sahihi ya wakazi," alisema.

Naye Diwani Laizer, alisema zahanati ni muhimu na kwamba anatambua shida inayowakabili wakazi hao na ameshafikisha jambo hilo kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ambayo kwa utaratibu ilio nao, itaongeza nguvu kwenye ujenzi huo utakapofikia hatua ya kufungwa lenta.

Awali, ilielezwa kuwa wananchi wa eneo hilo walikubaliana kuchangishana Sh. 10,000 kila kaya ili kujenga jengo la zahanati lenye huduma ya kliniki na wamefanikiwa kuanza ujenzi wa huo lakini kwa sasa unasuasua kutokana na kasi ndogo ya uchangaji.

Jengo la zahanati lililokusudiwa litakuwa na vyumba vitatu na maabara, na litakapokamilika litawezesha huduma za afya kutolewa kwenye mazingira mazuri.

Katika mkutano huo pia, kero nyingine zilizowasilishwa ni pamoja na ubovu wa barabara za mitaa, kudorora kwa kasi ya kuunganishwa kwa huduma ya maji na kukosekana kwa juhudi za kusaidia vikundi sahihi kupata mikopo kwa makundi maalum hasa vijana, wanawake na wenye ulemavu.

# Wadau wataka mabadiliko ya sheria na Katiba mpya

**Na Romana Mallya**

ZIKIWA zimebaki siku 16 kuelekea maadhimisho ya Siku ya Demokrasia Duniani, wadau wa siasa na wanaharakati wamesema, ni muhimu kufanya mabadiliko ya sheria ambazo nyingi zilitungwa wakati wa ukoloni na wakoloni pamoja na kuwa na Katiba mpya.

Pia, wamesema suala la usawa wa kijinsia bado haijaimarika vya kutosha kwa sababu wanawake si wengi kwenye ngazi za uongozi.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti kuhusiana na siku hiyo na nini kifanyike, wadau hao walisema sheria zilizopo zifanyiwe marekebisho kwa kuwa nyingi zilitungwa enzi za ukoloni na zimepitwa na wakati. .

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania, Onesmo Olengurumwa, alisema suala la demokrasia Tanzania bado ni changamoto ambayo inatakiwa kufanyiwa kazi kubwa.

"Tunapozungumza demokrasia tunaangalia mambo mengi. Demokrasia si uchaguzi, si kuwa na vyama vingi, si kuingia kwa uchaguzi huru na wa haki. Demokrasia ni ushirikishwaji mpaka wa wadau na wananchi katika kuamua mambo yao," alisema.

Serikali ya kidemokrasia, alisema ni ile ambayo ina mifumo, misingi, taasisi, sheria na katiba inaruhusu wananchi na taasisi zao kuwa huru na kushiriki katika mambo ya kitaifa.

"Hatuna katiba ambayo inapaswa kutumika kwenye nchi inayozungumza demokrasia. Katiba iliyopo ni ile iliyotengenezwa kipindi hakuna demokrasia. Bado tunabanwa na mfumo wa chama kimoja. Sheria nyingi zilitumwa kipindi cha ukoloni na wakati wa chama kimoja.

"Ndiyo maana mnaona vyombo vya habari vinakwama, asasi za kiraia zina changamoto, vyama vya siasa vimepata changamoto kubwa, hata taasisi tulizonazo zimejengwa katika misingi isiyo ya kidemokrasia. Ukiangalia Bunge na viongozi wanavyopatikana, ukiangalia upatikanaji wa majaji bado wanateuliwa na Rais, nchi nyingine wanaomba kama kazi," alisema.

Kuhusu nini kifanyike, Olengurumo alisema cha kwanza ambacho kitasababisha kutatua changamoto za kidemokrasia ni kuwapo kwa katiba mpya ya wananchi itakayoendana na mfumo wa demokrasia ya sasa.

Pia, alisema zibadilishwe sheria zote ili ziendane na mfumo wa vyama vingi na wa kidemokrasia na wananchi waelimishwe washiriki kwenye mambo ya msingi bila kubanwa.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema, alisema wanaamini demokrasia ni pamoja na haki za watu kukusanyika na kujumuika na kutoa maoni kwa uhuru.

"Hapa kwetu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa imezuiliwa kwa matamko na hivyo, haki hii haipo japo inalindwa na katiba iliyopo. Haki ya kuwajibisha viongozi wao ni sehemu ya demokrasia.

"Laiti wananchi wangekuwa na Katiba ambayo inatoa haki hii, leo wabunge wengi kama si wote wangeshaondolewa kutokana na kupitisha bajeti na sheria ya fedha ambayo imeongeza ugumu wa maisha sababu ya tozo ambazo wamepitisha. Tunahitaji katiba mpya ambayo itailinda demokrasia yetu," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Joyce Shebe, alisema hali ya demokrasia Tanzania inaimarika lakini si kwa kiwango kikubwa.

"Tunachojivunia tuna uchanguzi ambao tunafanya kila baada ya miaka mitano. Wananchi wanashiriki kuchagua viongozi ambao wanapenda kuwaweka madarakani ili wawatumikie. Hii inaleta matumaini kwa sababu yule aliyemaliza muda wake anatoka kwa utaratibu wa katiba, sheria na kanuni," alisema.

Kuhusu usawa wa kijinsia, alisema bado haijaimarika vya kutosha kwa sababu wanawake siyo wengi waliopo kwenye ngazi ya uongozi na kwamba changamoto zinaanzia kwenye vyama vya siasa, teuzi huwabeba zaidi wanaume.

"Tunachotamani kuona ni ule usawa demokrasia unaelezwa kwa jinsia zote wanawake kwa wanaume ya kusimama na kuongoza, kuteuliwa na kuchaguliwa, pia watu wote wanapata taarifa tunakwenda kwenye uchaguzi kuna fursa hii.

"Tanzania imeridhia mikataba mingi ya kimataifa ambayo inaongeza au kuchochea masuala ya demokrasia, hii inasaidia mihimili ya serikali kuzingatia hilo. Kuundwa kwa mashirika ya kiraia kama TAMWA, yanafanya kazi ya ziada kuisaidia serikali na jamii, yanatoa wigo kutoa elimu ya umuhimu wa kushiriki," alisema. .

Joyce, alisema kwa hali waliyonayo tangu Rais Samia Suluhu Hassan, ameshika madaraka mitazamo hasi ya kijamii ya kumwona mwanamke hawezi kuongoza imeanza kupungua na ameleta hamasa kwa wanawake.

Mwandishi wa Habari na mwanaharakati mashuhuri, Jenerali Ulimwengu, akizungumza na Haki TV iliyo chini ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kuhusu demokrasia Tanzania, alisema tangu mwaka 1992, hadi sasa hali ya kutotaka kuwa na ushindani wa kisiasa imeendelea.

"CCM inaogopa, wamevunja utaratibu wa kuwa na mazungumzo na mijadala na ukinzani ndani ya chama chao, hakuna ushindani ndani ya chama chao ukiangalia bungeni wapo peke yao, yale mazoea ya kupambanisha hoja hawana.

"Demokrasia inalindwa na mifumo ya kikatiba na kisheria, inapotokea kuwa mifumo ya kikatiba na kisheria inatoa mianya ya demokrasia kuminywa, hapo Haki za watu zinakosa ulinzi thabiti," alisema.

Alisema, wakati wanaelekea katika Siku ya Demokrasia Duniani, lazima wajiulize kama Katiba imeweka misingi imara ya kulinda demokrasia nchini.

# Wahalifu wavamia mtaa, wapora mali na kujeruhi

**Na Shufaa Lyimo**

WATU watano wamejeruhiwa huku mmoja akiwa mahututi baada ya kundi la vijana kuvamia mtaa wa Tagusako, Tabata jijini Dar es Salaam, kupora mali na fedha taslimu.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, mashuhuda na viongozi wa mtaa huo, walisema vijana hao wakiwa na silaha za jadi waliwakata kwa mapanga waendesha bodaboda watatu na wananchi wawili, huku wengine wakikatwa vidole.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Kata ya Tabata, Peter Joakimu, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 28, mwaka huu, majira ya saa tano usiku na kundi hilo la vijana lililokuwa limebeba silaha kama visu na mapanga.

Alisema wanamshikilia mtu mmoja ambaye alionekana na watuhumiwa hao.

"Kweli vijana hao walifanya uhalifu huo, waliwaumiza wananchi watatu pamoja na vijana wawili wa bodaboda ambao kati yao mmoja anafahamika kwa jina la Nelson Aruya (30), ambaye mpaka sasa hali yake sio nzuri amelazwa Hospitali ya Amana," alisema Joakimu. Mwenyekiti huyo alisema kundi hilo la wahalifu lilivamia maduka na kupora fedha na kuwanyang'anya simu za kiganjani wananchi.

Alisema walishirikiana na Kituo cha Polisi Tabata na kumpata mhusika mmoja ambaye majira ya mchana siku ya tukio, alionekana na watuhumiwa wengine nyumbani kwake.

Hata hivyo, alipofikishwa kituoni alibainika kuwa sio mkazi wa eneo hilo.

Mjumbe wa eneo hilo, Saida Mashine (60), alisema vijana hao walivamia eneo hilo mapema wakati baadhi ya wananchi wakiwa hawajafunga biashara zao. "Nilikuwa nipo ndani nikasikia kelele nje nilipotoka nikamkuta kijana mmoja wa bodaboda anatoka damu nyingi kichwani na mkononi, huku akiwa anapiga kelele anakimbia ikanilazimu nifanye utaratibu apelekwe hospitali huku nikiwa nimeishikilia pikipiki yake,"alisema Mashine.

Tukio hilo alidai limeathiri uchumi wa eneo hilo baada ya kuwapora wananchi fedha na mali zilizokuwa kwenye biashara zao.

Mmoja wa majeruhi, aliyekatwa mapanga kichwani na kukatwa kidole cha mkono Abduli Salum Maketa (35), alisema vijana hao walimvamia akiwa anashusha abiria na kupora simu na fedha alizokuwa nazo.

Naye dada wa majeruhi, Sara Aruya, alisema hali ya mdogo wake sio nzuri anaendelea na matibabu Hospitali ya Amana.

"Nelson hali yake sio nzuri alikatwa mapanga mawili kichwani vile vile alikatwa kidole cha mkono ninavyokuambia hata kuongea kwake ni kwa shida, tunaomba serikali isimamie jambo hili kusudi hawa wanaofanya uhalifu huu wadhibitiwe," alisema.

Shuhuda mwingine Sofia Hamisi, alisema alikuwa anaelekea nyumbani na kuvamiwa na vijana hao ambao walimpora simu na kutishia kumchoma kisu.

Kutokana na tukio hilo baadhi ya wananchi wamedai kuhofia kutoka nje, huku wakiliomba jeshi la polisi kuimarisha ulinzi kutokana na kuongeza kwa matukio ya uhalifu.

Kaimu Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Willium Mponda, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa askari wanawasaka waliohusika na wanawashikilia watu kadhaa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NA. 624/2021**

**WINDING UP NIT LOGISTIC AND**
**ENGINEERING COMPANY ............................................. MDAI**

**VERSUS**

**NIT LOGISTICS AND**
**ENGINEERING COMPANY.......................................... MDAIWA**

**Kwa:**

**NIT LOGISTICS AND**
**ENGINEERING COMPANY.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Mdai tajwa hapo juu amefungua maombi ya kufunga kwa kampuni kwa yeyote mwenye maslahi na kufungwa kwa kampuni hii unatakiwa kufika katika Mahakama hii tukufu anayetambulika kisheria tarehe 01/09/2022 saa 4:00 asubuhi ili kuwasilisha maslahi yako.

Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unataraji kuvitumia katika maombi haya.

**KUMBUKA KUWA:** Usipohudhuria siku hiyo na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito huu, mahakama itaamuru utekelezaji kuendelea.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 25 mwezi Agosti, 2022.

**NAIBU MSAJILI**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**

217020002

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

## TAARIFA KWA UMMA

### MAUDHUI YASIYOENDANA NA MAADILI YA KITANZANIA

Kwa mujibu wa sheria Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imepewa jukumu la kusimamia maudhui yote yanayorushwa na vituo vya Utangazaji pamoja na mitandao ya ki-elektroniki.

Siku za hivi karibuni, kumekuwa na taarifa inayosambazwa na baadhi ya watumiaji wa mitandao ya Kijamii ikitahadharisha juu ya uwepo wa maudhui ya televisheni kwenye vipindi vya watoto yaliyo kinyume na Sheria, Kanuni za Utangazaji, Maadili na Miiko ya utangazaji nchini.

TCRA ingependa kuuhakikishia umma kuwa vipindi vya maudhui vyote vinayorushwa na vyombo vya Utangazaji hapa nchini huhakikiwa kwanza na pia kufuatiliwa ili kujiridhisha kuwa yanazingatia Sheria, Kanuni, Maadili na Utamaduni wa Mtanzania.

TCRA imejiridhisha kuwa hakuna chombo cha Utangazaji kilichorusha maudhui hayo yasiyofaa kwa watoto. Hata hivyo, TCRA inavikumbusha vyombo vyote vya Utangazaji kuendelea kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na Masharti ya Leseni ya Utangazaji kwa kuhakikisha vituo vyao haviendi kinyume na maadili ya kitanzania.

Aidha, TCRA inaendelea kusisitiza kuwa wajibu wa kuwalinda Watoto kutokana na maudhui yasiyofaa hasa kwenye mitandao ya kijamii ni wa kwetu sote ikianzia kwa Wazazi, Walezi na Mashuleni ambapo Watoto wetu hutumia muda mwingi huko wakiwa masomoni.

Pia TCRA inaiasa jamii kutosambaza katika mitandao ya kijamii jumbe zinazoleta taharuki, upotoshaji na hofu katika jamii. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wale wote watakaobainika kusambaza jumbe hizo. TCRA inafuatilia kwa ukaribu maudhui yanayowekwa kwenye mitandao. Kwa yeyote atakayebainika kuweka na kusambaza habari za upotoshaji mitandaoni, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**IMETOLEWA NA MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
**TAREHE 29/08/2022**

2170212102

# Afariki dunia akijaribu kujiokoa katika moto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

REHEMA Chande (70), mkazi wa Mji Mkongwe mjini Unguja, amefariki dunia baada ya kujaribu kujiokoa na mjukuu wake kutokana na moto uliozuka katika nyumba wanayoishi mji Mkongwe.

Mama huyo amepoteza maisha baada ya kujirusha katika ghorofa akiwa yeye na mjukuu wake wakati wakijihami na moto.

Tukio hilo lilitokea jana majira ya asubuhi katika Shehia ya Kiponda, Mji Mkongwe, lakini mjukuu wake, Nabil Issa Ramadhan, miaka mitano amepata majeraha.

Akisimulia ilivyotokea jirani wa bibi huyo, Seif Omar Othman, alisema alitoka ndani kunawa uso ndipo akaona moto umeanza kuwaka ndani kwa Rehema na kuanza kumgongea mlango ili atoke.

Seif alisema wakati moto ukiendelea kuwaka alimgongea mlango jirani yake huyo ili kujihami lakini mlango ulikuwa umefungwa na bibi huyo alichupa kupitia dirishani baada ya mlango kuwaka moto.

"Baada ya kuruka chini alipoteza maisha huku mjukuu wake akiwa amejeruhiwa na kukimbizwa (kupelekwa) katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

Jirani mwingine anayeishi kwenye jengo hilo, Khadija Omar, alisema kama mlango wa bibi huyo usingekuwa umefungwa pengine wangemwokoa maana walitumia muda kidogo wakiangalia namna ya kumwokoa

Sheha wa Shehia hiyo, Juma Khamis Makame alisema bibi huyo alikuwa anaishi na mjukuu wake na watoto wengine lakini kwa wakati huo hawakuwa ndani.

Kamanda wa Kikosi cha Zimamoto Zanzibar, Rashid Mzee Abdallah, alisema walipofika eneo la tukio walimkuta bibi huyo na mjukuu wake lakini walipofikishwa hospitalini daktari alisema tayari Rehema ameshafariki dunia.

"Huyu Bi Rehema aliruka kujiokoa na moto baada ya kutanda na kushindwa kutoka ndani. Kwa hiyo aliporuka yeye kapoteza maisha lakini bahati nzuri mjukuu wake kajeruhiwa na yupo anaendelea na matibabu," alisema.

Kuhusu athari zingine, Mkuu huyo wa Kikosi cha Zimamoto, alisema bado wanaendelea na kazi ya kuuzima kutokana mazingira ya eneo hilo kutokuwa rafiki.

"Kama unavyoona mazingira ya Mji Mkongwe yalivyo ni magumu kidogo na tumekuwa tukisema jambo hili kila mara namna ya kuweka mazingira mazuri yanapotokea majanga kama haya ili kudhibitiwa," alisema.

Kamanda huyo alisema licha ya mazingira kutokuwa rafiki, kuna miundombinu ya kuwapo visima vya maji kwa ajili ya kuzimia moto, hivyo wameunganisha mabomba kutoka kwenye visima hivyo.

Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Msaraka, alisema licha ya kuwapo visima hivyo zaidi ya 330, maji yake hayana kasi kwa sababu tayari wananchi wameingilia miundombinu hiyo na kujiunganishia maji kwa matumizi ya nyumbani.

Alisema kuna haja ya kutatua changamoto hizo kwa kuboresha huduma za maji na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kufanya operesheni za mara kwa mara ili kuweka miundombinu yao katika hali ya usalama.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mustapha Kitwana, alisema baada ya kukamilika kwa shughuli hiyo kamati ya ulinzi na usalama itafanya tathmini kubaini athari zilizojitokeza huku akiagiza Sheha wa shehia hiyo kuchukua idadi ya familia zilizokuwa zikiishi kwenye jengo hilo.

# Bunge lataka NHC kuongeza kasi ukusanyaji madeni sugu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji ya Mitaji ya Umma (PIC), imeliagiza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuongeza kasi ya ukusanyaji wa madeni kwa wadaiwa sugu wa shirika hilo.

Imeelezwa kuwa hadi Desemba, mwaka jana, kulikuwa na madeni ya Sh. bilioni 26 ya wadaiwa sugu wa shirika hilo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa, alisema pamoja na kazi nzuri inayofanywa na shirika hilo, wameagiza kasi ya kudai madai hayo iongezwe.

"Tumeagiza kwenye madeni kasi iongezwe ya kudai kwa wateja kwa ajili ya maendeleo zaidi ya shirika," alisema.

Silaa pia alisema maagizo yaliyotolewa na kamati hiyo mwaka jana yametekelezwa kwa asilimia 100.

"Shirika limeendelea na ujenzi wa nyumba kwenye miradi iliyokuwa imesimama kama Kawe na Morocco ambayo Watanzania wamekuwa wakipita na kuiona kuwa miradi imekaa muda mrefu," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kwa sasa shirika hilo limekuja na mikakati ambayo kamati imeridhika na mpango ambao unatekelezeka vizuri. Pia alisema kamati imeipongeza NHC kwa kutumia faida kufanya uwekezaji.

"Tumeona mikakati ya nini wanatarajia kufanya na mpango kwa miradi mipya au iliyokuwepo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NHC, Dk. Sophia Kongela, alisema maelekezo ya awali yaliyotolewa na kamati yalikuwa kujenga nyumba kwa gharama nafuu na kuhakikisha kodi inakusanywa jambo ambalo limeendelea kutekelezwa.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Nehemia Mchechu, alisema shirika linaendelea kuhakikisha madeni yanakusanywa na kuangalia mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya nyumba za Watanzania.

**TANGAZO**

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

# PRESIDENT'S OFFICE- REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

# BUKOMBE DISTRICT COUNCIL

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30TH JUNE 2021

| | NOTE | 2021 TZS ('000) | RESTATED 2020 TZS ('000) |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| Cash and Cash Equivalent | 20 | 1,072,232 | 2,031,203 |
| Receivables | 21 | 186,879 | 108,038 |
| Loans Receivables | 22 | 379,321 | 282,771 |
| Prepayments | 23 | 201,388 | 58,190 |
| Inventories | 24 | 207,908 | 335,663 |
| Investments in LGLB: LGAs To LGLB | 27 | 41,316 | 41,316 |
| Property Plant and Equipment | 25 | 28,978,094 | 27,188,000 |
| Biological Assets | 26 | 34,042 | 34,042 |
| **TOTAL ASSETS** | | **31,101,180** | **30,079,223** |
| **LIABILITIES** | | | |
| Payables and Accruals | 28 | 848,617 | 441,359 |
| Deposit - Others | 29 | 258,421 | 204,193 |
| Other Borrowings by Government Entities | 30 | 1,074,200 | 1,092,600 |
| Employee Benefits Liabilities | 31 | 2,609,019 | 1,812,506 |
| Deferred Income (Recurrent) | 32 | 196,005 | 162,252 |
| Deferred Income (Development) | 33 | 744,422 | 1,598,619 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **5,730,684** | **5,311,529** |
| Net Asset | | **25,370,496** | **24,767,694** |
| **NET ASSETS/EQUITY** | | | |
| Other Reserves | | 41,316 | 41,316 |
| Accumulated surpluses/(deficits) | | 25,329,180 | 24,726,378 |
| **TOTAL NET ASSETS/EQUITY** | | **25,370,496** | **24,767,694** |

**Lutengano George Mwalwiba**
**District Executive Director**

Date 31/03/2022
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR BUKOMBE

**Yusuph Mohamed**
**Council Chairperson**

Date 31/03/2022
MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA BUKOMBE.

## STATEMENT OF FINANCIAL PPERFORMANCE FOR THE YEAR 30TH JUNE 2021

| | NOTE | 2021 TZS ('000) | RESTATED 2020 TZS ('000) |
|---|---|---|---|
| **REVENUE** | | | |
| Revenue From Exchange Transactions | 7 | 191,082 | 355,628 |
| Levies | 8 | 580,408 | 687,526 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 9 | 1,061,525 | 1,108,995 |
| Other Revenue | 10 | 25,058 | 36,538 |
| Subvention From Other Government Entities | 11 | 28,155,556 | 25,211,614 |
| **TOTAL REVENUE** | | **30,013,629** | **27,400,301** |
| **EXPENSES AND TRANSFERS** | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 12 | 22,227,616 | 21,524,038 |
| Supplies and Consumables Used | 13 | 3,545,129 | 3,716,493 |
| Routine Repair and Maintenance Expenses | 14 | 1,120,245 | 860,131 |
| Social Benefits | 15 | 767,734 | 196,016 |
| Finance Costs | 16 | 58,800 | 101,881 |
| Other Expenses | 17 | 255,518 | 666,787 |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 18 | 1,393,127 | 909,611 |
| Impairment of Receivables | 19 | 42,658 | 48,160 |
| **TOTAL EXPENSES AND TRANSFERS** | | **29,410,827** | **28,023,117** |
| Share of Deficit of Associates and Joint Ventures | | - | - |
| **Surpluses/deficits for the period** | | **602,802** | **(622,816)** |

**Lutengano George Mwalwiba**
**District Executive Director**

Date 31/03/2022
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR BUKOMBE

**Yusuph Mohamed**
**Council Chairperson**

Date 31/03/2022
MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA BUKOMBE.

## STATEMENT OF CASH FLOW FOR THE YEAR 30TH JUNE 2021

...H JUNE, 2021

| | NOTES | 2021 TZS ('000) | RESTATED 2020 TZS ('000) |
|---|---|---|---|
| **CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | | |
| **RECEIPTS** | | | |
| Subvention from Other Government Entities | 11 | 26,207,882 | 25,948,367 |
| Revenue from Exchange Transactions | 7 | 191,220 | 170,660 |
| Other revenue | 10 | 13,446 | 3,825 |
| Levies | 8 | 589,145 | 688,254 |
| Increase in deposits | 29 | 54,226 | 67,505 |
| Fees, fines, penalties and Forfeits | 9 | 985,812 | 1,340,255 |
| **Total Receipts** | | **28,041,733** | **28,218,866** |
| **PAYMENTS** | | | |
| Wages,Salaries and Employee Benefits | 12 | 21,431,103 | 21,649,471 |
| Supplies and consumables paid | 13 | 2,605,378 | 3,668,367 |
| Social Benefits | 15 | 767,734 | - |
| Routine repair and maintenance paid | 14 | 852,542 | 623,977 |
| Other Expenses | 17 | 255,518 | - |
| Finance cost | 30 | 3,000 | 3,300 |
| **Total Payments** | | **25,915,275** | **25,945,115** |
| **Net CashFlow from Operating Activities** | | **2,126,458** | **2,273,751** |
| **CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | | |
| Investing Activities | | | |
| Receipt from Loan Issued | 22 | 137,086 | 62,132 |
| Loan Issued | 22 | (233,636) | (186,459) |
| Acquisition of property, plant, and equipment | 34 | (2,970,837) | (901,933) |
| Acquisition of biological assets | | - | (34,042) |
| **Total Investing Activities** | | **(3,067,387)** | **(1,060,302)** |
| **CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES** | | | |
| **Financing Activities** | | | |
| Cash proceeds from borrowings | | (17,000) | (20,999) |
| **Total Financing Activities** | | **(17,000)** | **(20,999)** |
| **Net Increase / Decrease in Cash** | | **(957,929)** | **1,192,450** |
| Effect of Foreign Currency Changes | | - | - |
| Cash to be surrendered to Holiding Account | | - | - |
| Cash to be surrendered to MOF | | (1,042) | (7,981) |
| Cash and cash equivalent at beginning of period | | 2,031,203 | 846,734 |
| **Cash at the end of period** | 20 | **1,072,232** | **2,031,203** |

**Lutengano George Mwalwiba**
**District Executive Director**

Date 31/03/2022
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR BUKOMBE

**Yusuph Mohamed**
**Council Chairperson**

Date 31/03/2022
MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA BUKOMBE.

35

## 1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

Hon. Chairperson of the Council,
Bukombe District Council,
P.O. Box 2,
Bukombe.

### 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Opinion**

I have audited the financial statements of Bukombe District Council which comprise the statement of financial position as at 30 June 2021, and the statement of financial performance, statement of changes in net assets and cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position Bukombe District Council as at 30 June 2021, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, Cap.290 (R.E. 2019).

**Basis for Opinion**

I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the Audit of the financial statements section of my report. I am independent of Bukombe District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

**Key Audit Matters**

Key audit matters are those matters that, in my professional judgment, were of most significance in my audit of the financial statements of the current period. I have determined that there are no key audit matters to communicate in my report.

Salhina M. Mkumba
Ag.Controller and Auditor General,
Dodoma, United Republic of Tanzania.
March, 2022

217019702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nyongeza ya siku 7 sensa ikalete chachu kuhesabiwa

**SENSA** ya Watu na Makazi ni mchakato wa kitaifa unaofanyika kila baada ya miaka 10 na ya mwisho kufanyika nchini ilikuwa mwaka 2012.

Sensa ya mwaka huu iliyoanza Agosti 23, ni ya sita kufanyika nchini baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Sensa nyingine zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

Juzi, Kamisaa wa Sensa Kitaifa, Anne Makinda, alitangaza kuongezwa siku saba katika mchakato wa kukamilisha Sensa ya Watu na Makazi na kueleza mchakato huo utakamilika Septemba 5.

Sababu kuu ya kuongezwa kwa siku hizo ni kuwafikia Watanzania wote na kufanyika kwa sensa ya majengo ambayo imeanza jana.

Pia, hadi kufikia juzi saa 2:00 asubuhi idadi ya Watanzania waliohesabiwa walifikia asilimia 93.45, huku waliosalia wakiwa ni asilimia 6.5.

Tunatoa pongezi kwa serikali kwa kuwezesha kuifikia idadi hiyo ya Watanzania ni imani yetu kwa siku hizo zilizoongezwa kila Mtanzania anakwenda kuhesabiwa.

Pia, tunapongeza hatua hiyo ya kuongeza muda wa kukamilisha mchakato huo kwa sababu idadi kubwa ya Watanzania ilikuwa na kilio cha kutofikiwa na makarani wa Sensa ya Watu na Makazi.

Tunaamini kwamba kuongezwa kwa siku hizo kutakamilisha mchakato huo muhimu kwa mustakabali wa taifa na maendeleo kwa wananchi wote.

Hivyo, kuongezwa kwa siku hizo kuwaamshe makarani ambao kwa namna moja ama nyingine walikuwa na kasi ndogo ya kuchukua takwimu za wananchi.

Sasa makarani wanapaswa kuchangamka, kuhakikisha wanapita mtaa kwa mtaa, nyumba kwa nyumba kuchukua takwimu muhimu zinazohitajika.

Katika siku hizo saba elimu zaidi itolewe kwa Watanzania ambao walikuwa wamegoma kuhesabiwa, busara na hekima zitumike kuwaelimisha umuhimu wa kupata takwimu za wananchi.

Ni imani yetu kwamba kuongezwa kwa siku hizo pia kutawaamsha baadhi ya Watanzania ambao wakati wa kuanza kwa mchakato huo Agosti 23, mwaka huu, walikuwa na majukumu mengine waliyokuwa wakiyafanya, kusababisha kutohesabiwa.

Kila Mtanzania ambaye hakupata fursa ya kuhesabiwa wakati mchakato huo umeanza ni wakati muafaka kwa sasa kwa wao kuhesabiwa kwa manufaa ya taifa.


Sote tunafahamu kwamba umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi ni pamoja na kuisaidia serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, mageuzi ya masuala ya afya na jamii, pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa.

Faida nyingine ni taarifa za watu husaidia katika mamlaka za wilaya katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali.

Faida nyingine ni takwimu zitakazokusanywa zitaiwezesha serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine, ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira.

Mwisho, tunatoa rai kwa Watanzania wenye tabia ya kutoa taarifa za uongo kwa makarani kuacha mara moja kwani takwimu sahihi zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi na kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Msajili angemaliza viporo migogoro ya CUF, NCCR

**SASA** ni zaidi ya miezi tisa tangu Chama cha CUF kiingie kwenye mgogoro wa kiuongozi uliosababisha baadhi ya makada wake kuvuliwa uanachama na baadhi yao kukimbilia ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa kutafuta haki.

Wakati uamuzi wa kuhusu mgogoro wa CUF ukiwa haujatolewa, ukaibuka mwingine ndani ya Chama cha NCCR- Mageuzi ambao nao umefikishwa katika ofisi hiyo na kuifanya iwe na viporo viwili vya migogoro.

Ucheleweshaji wa majibu wa mgogoro wa CUF, umesababisha kuwapo kwa malalamiko kutoka kwa wale walioupeleka katika ofisi hiyo wakidai kuwa kuna mchezo wa kutaka kulinda vigogo wa chama hicho.

Hata hivyo, majibu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambayo yamekuwa yakitolewa mara kwa mara ni kwamba, inachukua kila hatua za kuhakikisha uamuzi unaotolewa unakuwa wa haki kwa pande zote.

Kwamba, ofisi hiyo ni mlezi wa vyama na wanachama wake, hivyo inafanya kazi wa kufuata, sheria, kanuni na taratibu zilizoipa jukumu hilo na sio matakwa ya kikundi au watu fulani, huku ikitaka wahuskia kuwa wavumilivu.

Ni kweli kinachosemwa na ofisi hiyo kina mashiko, lakini ingekuwa ni vyema kuongeza kasi ya kupitia malalamiko hayo ili kuondoa mawazo yaliyojengeka kwamba Ofisi ya Msajili inafanya hivyo kuwalinda vigogo wa CUF.

Ninadhani hatua ya kumaliza mgogoro huo zikichukuliwa haraka, itasaidia kupunguza viporo vya migogoro ya vyama katika ofisi, kwani mbali na huo wa CUF kuna mwingine wa Chama cha NCCR- Mageuzi.

Mgogoro wa NCCR- Mageuzi, unaelezwa na Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi kuwa anasubiri kwanza majibu ya Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu- Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene.

Akakiri kwamba, ofisi yake ilipokea mgogoro huo, lakini ghafla viongozi wa chama waliosimamishwa, wakaenda pia kwa Waziri, hali iliyomlazimu asubiri kwanza uamuzi wa Waziri huyo ndipo ajue pa kuanzia.

Hilo ninakubaliana naye kwamba, ofisi yake kwa sasa haina cha kufanya kuhusu mgogoro huo zaidi ya kusubiri maelekezo ya Waziri, lakini pamoja na hayo, ingeharakisha kumaliza mgogoro wa CUF.

Ninaamini kwamba, iwapo itafanya hivyo, inaweza kuwafanya wale waliofukuzwa ndani ya chama kujua hatma yao kama wanarudishwa au wanatoswa moja kwa moja, ili wajue ni hatua gani zaidi wachukue.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni mlezi wa vyama, njia nzuri ambayo ingesaidia kuvifanya visiwe na migogoro, ni kuharakisha kutoa uamuzi inapofikishiwa malalamiko ya wanachama.

Ikumbukwe kuwa kumekuwapo na madai kwamba, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inalea migogoro ya vyama, hivyo ili kuondoa madai hayo, ninadhani njia nzuri ni kuhakikisha malalamiko yanashughulikiwa haraka.

Suala la kujipa muda kushughulikia migogoro ni la muhimu, lakini pia ninadhani isingefaa muda uwe mrefu sana kama ambavyo imetokea kwa mgogoro wa kiuongozi wa Chama cha Wananchi (CUF).

Wanachama waliofukuzwa, wanadai kuwa mgogoro wao umechukua muda mrefu bila kutolewa uamuzi na wakati wakiendelea kusubiri majibu, umejitokeza mwingine wa Chama cha NCCR- Mageuzi.

Meza ya mazungumzo inatajwa kama ndiyo njia nzuri ya kumaliza migogoro katika vyama vya siasa, hivyo ninaamini hatua ya wanachama kukimbilia ofisi hiyo, inalenga kutaka kumaliza migogoro katika vyama vyao.

Msajili wa Vyama vya Siasa alishawahi kutumia njia hiyo alipoitisha meza ya mazungumzo ya Baraza la Vyama vya Siasa kujadiliana na wadau wa siasa na maendelo nchini, baada ya kuwapo sintofahamu ndani ya vyama vya Siasa.

Ninadhani njia hiyo pia ingetumika kumaliza mvutano uliopo ndani ya CUF ulioanza Novemba mwaka jana, ingawa unaonekana kwenda kimya kimya, huku waliofukuzwa wakilalamikia ofisi hiyo, lakini na huo mpya wa NCCR.

HABARI KITAIFA

## Shaka apongeza jitihada za Rais Samia uwekezaji DIT

Na Mwandishi Wetu



KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, (Pichani) amesema Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeridhishwa na hatua zinazochukuliwa na serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan katika uwekezaji katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT).

Shaka ametoa pongezi baada ya serikali kuiwezesha taasisi hiyo kutekeleza mradi wa ujenzi wa vituo vya umahiri kwa kupatiwa ya Sh. bilioni 100.

Akizungumza juzi baada ya kufanya ziara fupi DIT, Shaka alisema wamekuwa wakienda maeneo mbalimbali kukagua na kuangalia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020- 2025 katika mashirika na taasisi ambazo zimepewa dhamana na serikali lakini kilichofanyika katika taasisi hiyo ni cha mfano wa kuigwa.

"Kumekuwa na jitihada kubwa zinazofanywa na CCM kupitia serikali kwenye uwekezaji wa fedha nyingi za maendeleo maeneo mbalimbali. Moja ya maeneo ambayo pengine hatujafika kuona namna ambavyo fedha zimewekwa na utekelezaji unaendelea, ni eneo hili lililobeba teknolojia.

"Nikisema teknolojia tunamaanisha mfumo mzima wa mabadiliko haya ya kidunia na hapa nazungumzia TEHAMA (teknolojia ya habari na mawasiliano) na leo tumepata fursa hii kuona namna ambavyo wenzetu wa DIT wanatumia utaalamu huu kubadilisha miundombinu hii ya magari kutoka kwenye mafuta kwenda kwenye gesi," alisema.

Naye Mkuu wa DIT, Prof. Preksedis Ndomba, alisema wanaishukuru serikali kwa kufanya uwekezaji mkubwa kwenye taasisi hiyo na kazi iliyoko mbele yao ni kuhakikisha wanatekeleza miradi ya ujenzi wa vituo vya umahiri.

Prof. Ndomba alitumia nafasi hiyo kuelezea kwenye ufungaji wa mifumo ya kutumia gesi kwenye magari wameendelea na sasa wameshafunga kwenye magari 1,000 na miongoni mwao yamo ya serikali.

# Sensa ya majengo yakubalika Dar

Na Waandishi Wetu

BAADHI ya wananchi kwenye mitaa mbalimbali jijini Dar es Salaam, wameeleza kuridhishwa na sensa ya watu na makazi na sasa wako tayari kushiriki ya majengo iliyoanza jana.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mwenge, Bashir Hozza, alisema kwa wananchi wa eneo hilo wamehesabiwa asilimia 98 na kwamba kwa siku ya jana makarani waliendelea na kazi bila kikwazo.

"Wananchi wana uelewa kuhusu zoezi hili kwa sababu tumejitahidi kuwaelimisha kilichobaki ni utekelezaji na nimepata bahati wananchi wengi wa Mwenge ni waelewa ,"alisema Hozza ambaye pia ni Mwenyekiti wa Wenyeviti Kata ya Kijitonyama.

Aidha, alisema maswali ni ya kawaida na kwamba wanalenga kujua tofauti ya nyumba kama ni ya tofali au makuti, imeezekwa au vigae na kama ni ya biashara.

Kwa mujibu wa Hozza, ni muhimu serikali kuhakikisha makarani hao wanalipwa stahiki zao kwa wakati na utimilifu, ili kutoharibu kazi hiyo muhimu kwa taifa.

"Ilitakiwa watoe muongozo juu ya malipo kama ni baada ya kuhesabu watu au tutalipa nusu ya posho, wengine wanategemewa na familia zao wanaporudi nyumbani bila fedha inaonekana ni wababaishaji. Serikali iwe na kauli moja kama watu wanapewa wapewe au kama watu watapewa baada ya zoezi wajuwe ili kuepusha changamoto," alisisitiza Hozza.

Naye, mkazi wa Mwenge, Asha Juma, alisema: "Mpaka kufikia sasa zoezi la sensa ni zuri hususani mtaa wangu wote tumeshahesabiwa siku zile za mwanzo, na kwa sasa ni zoezi la makazi na majengo ndo ambalo linaendelea na nitatoa ushirikiano wakutosha juu ya hili pia, tayari nishawaona makarani hapa mtaani," alisema.

"Mimi naunga mkono kuhesabu makazi na majengo ina manufaa kwa nchi yangu katika kutambua idadi ya makazi na majengo hivyo basi nitatoa ushirikiano wa kutosha kama ule ambao nimetoa hapo awali katika kufanikisha hili," alisema Seif Matola, mkazi wa Mwenge.

Naye, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Ali Hassan Mwinyi, Kata ya Mikocheni, Bernard Rweyabula aliwataka wananchi ambao hawajahesabiwa kutumia siku za nyongeza kupata haki ya msingi.

Ofisa mtendaji wa kata hiyo, Hawa Salum alisema wanaendelea kupokea makarani wanaoendelea kuwahesabu huku wakipongeza siku zilizoongezwa.

Naye Dayana Dismass alisema serikali imefanya vizuri kuongeza siku hizo kwani kuna baadhi ya wananchi hawakukuweza kufikiwa.

**Imeandikwa na Beatrice Mwaigomole (SAUT), Loyce Cyriacus SJMC), Camila Bonanza, Owen Bariki na Fatuma Athumani (TUDARCo).**


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KARIAKOO | IDDI MUSA MLETE | NYUMBA | IDDI MUSA MLETE | VINGUNGUTI | 14/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| KARIAKOO | OMARI SAIDI MAINGO | NYUMBA | OMARI SAIDI MAINGO | TAMBANI-MKURANGA | 15/09/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | 1.NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA 2.1.NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.1123 KITALU 'L' HATI NAMBA 85726-MBAGALA 3.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO-CHAMAZI DOVYA | AHMAD KASSIM OMARY | 1.KIBAMBA 2.MBAGALA 3.CHAMAZI DOVYA | 15/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | KHALIDI RAI MWARAI | NYUMBA 2 ZENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK002736 NA TMK040337 | KHALIDI RAI MWARAI | MBAGALA KUU | 16/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | FRANK FRANK MUSHI | NYUMBA | FRANK MUSHI | BOCHELA-NKUHUNGU | 14/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | BEATHA JEROME SHIYO | NYUMBA YENYE HATI NO.35152-DLR | BEATHA JEROME SHIO | WEST CHINANGALI-DODOMA | 15/09/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | WORKING MACHINES DODOMA | MASHINE, 1.CUTTING MACHINE SLOUGH-DRILL S/N.1305 2.CUTTING MOTOR MACHINE S/N.YL-100L1-4 3.WELDING MACHINE S/N. CV-240 4.POWER TOOL S/N. DDG-150 5.ELECTRIC CUT-OFF MACHINE S/N. CO-355DC | DAVID JOHN NCHIMAN | DODOMA | 16/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ALEX LEOPORD RUEBANGILA | GARI TOYOTA ALPHARD T231 DPP | ALEX LEOPORD RUEBANGILA | SINZA | 15/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA (2) | MPOKI BROWN MWAIPASI | GONGOLAMBOTO NA KILUNYA | 15/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBEYA | ROGIMWA AGRO COMPANY LIMITED | KIWANJA CHENYE HATI NAMBA 083KYL/1204 | ROGGERS GIDION MWAMENGO NA ANNA DANIEL SANGA | ITETE KYELA MBEYA | 20/09/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MBEYA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.KIWANJA KIPO SONGWE 2.NYUMBA (3) ZIPO CHUNYA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.SONGWE 2.CHUNYA | 21/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MAGWE EMMANUEL WAMBURA | VIWANJA VITATU VYENYE HATI MILIKI NAMBA 54154,54140,54155 KITALU 'A' ILALILA | MAGWE EMMANUEL WAMBURA | ILALILA-BUSWELU | 15/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | OBEDI ZIHIRWADI MSINGA | NYUMBA | OBEDI ZIHIRWANI | KONGOWE-KIBAHA | 15/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MAIN | INTERCITY BUILDERS LIMITED | DOLL 3DSAK42 TRAILER NO. T984 DAH AND SDLG ROAD ROLLER NO. T423 DBV | INTERCITY BUILDERS LIMITED | CHANIKA | 26/09/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MAIN | WOODFIRST ENTERPRISE LIMITED | GARI TOYOTA LAND CRUISER PRADO NO. T.549 CRU | ALEXANDER ANSELIMI MUSHI | MAGOMENI | 20/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | BARAKAELI KUNDANDUNI MBISE | NYUMBA | BARAKAELI KUNDANDUNI MBISE | KING'ORI-ARUMERU | 15/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | NYUMBA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | MOSHONO | 16/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ARUSHA | MASANJA JAMES WANNA | KIWANJA | MASANJA JAMES WANNA | TERRAT ARUSHA | 20/09/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ARUSHA | RICHARD GABRIEL PALLANGYO | NYUMBA | RICHARD GABRIEL PALLANGYO | MAJI YA CHAI -ARUSHA | 21/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MAGRESTH RHOBI SASI | NYUMBA | MAGRESTH RHOBI SASI | MBONDOLE MSONGOLA | 14/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | KAIMU SAID AMANZI | NYUMBA | KAIMU SAID AMANZI | MVULENI-MSONGOLA | 16/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | AMRI BAKARI MAKANYA | NYUMBA | MWANAHAMISI KASSIM YUSUPH | KITUNDA | 14/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | RASHID SAID NGOMBO | NYUMBA | RASHID SAID NGOMBO | GOGO-ZINGIZIWA CHANIKA | 14/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | ISMAIL ISSA MICHAEL | NYUMBA | ISMAIL ISSA KASANGA | CHANIKA | 16/09/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | MNANDALA SAIDI MSAFIRI | NYUMBA | MNANDALA SAIDI MSAFIRI | PUGU | 20/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MARIAM SAIDI TUMBO | NYUMBA | DAHIMU KASSIMU CHKWAWA | YOMBO DOVYA | 14/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | RASHID SELEMANI RASHID | NYUMBA | MOHAMEDI ABDUL ATHUMAN | CHAMAZI | 15/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEGETA | BUMERA LODGE AND CO. LTD | NYUMBA | JOACHIM HERONIMUS MWINGIRA | MTAA WA KIGOGO KATI | 15/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | YASINI MBAGO MOHAMED | NYUMBA | YASINI MBAGO MOHAMED | PUGU BANGULO | 20/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JENEROSE ANNA LUZWILO | NYUMBA | JANE ANNA LUZWILO | BUZA | 15/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | BAHATI JAMES MAGOTI | NYUMBA | BAHATI JAMES MAGOTI | MBAGALA KILUNGULE | 16/09/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | NYUMBA | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | YOMBO VITUKA-SIGARA | 21/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ZULFA SHAFII MALENDA | NYUMBA | HALIMA SHAFII MALENDA | NZASA -CHARAMBE | 22/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MWANNE HASSAN SULEIMAN | NYUMBA | MWANNE HASSAN SULEIMAN | MAMBOLEO-SANDALI TEMEKE | 23/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | RAMADHANI SHABANI LIKIMANGIZA | NYUMBA | RAMADHANI SHABANI LIKIMANGIZA | CHARAMBE | 22/09/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; Tupigie simu **No. 0714939933/0718038313/0743885084/0754497396/0762260787/0752360133/0754376493/0754555654/0718038313/0719351040**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

217021602

# Vodacom yapongezwa kwa kuwekeza kwenye teknolojia

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, ameipongeza kampuni ya Mtandao wa Simu za mkononi ya Vodacom kwa kuwa mstari wa mbele kwenye kuleta mabadiliko yanayoigusa jamii moja kwa moja, hali inayochangia maendeleo kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana alipotembelewa na washindi wa bajaji na pikipiki kupitia kampeni ya 'M Pesa imeitika', Gondwe alitanabaisha kwamba Vodacom imekuwa kinara katika mapinduzi ya teknolojia na huduma zinazonufaisha Watanzania.

"Ni wakati mzuri kutumia mtandao ambao ni mzuri na wenye kutoa huduma kwa wakati kwa ajili ya kupanua wigo wa mawasiliano kwa namna moja ama nyingine," alisema.

Baadhi ya washindi wa zawadi za bajaji na pikipiki kupitia kampeni ya M-Pesa Imeitika, Magdalena Magoma na Beata Madachi, waliishukuru serikali kwa kuweka mazingira wezeshi yanayoziwezesha sekta binafsi na kampuni kama Vodacom kuweza kuchangia maendeleo ya vijana kama wao na jamii kwa ujumla.

Aidha, alisema huduma hiyo imewafikia vijana kutengeneza ajira kupitia pikipiki na bajaji ambazo zitaleta mabadiliko kwenye maisha yao na kuwawezesha kuchangia uchumi binafsi na wananchi.



Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Vodacom, Roseline Mworia (katikati), akishuhudia wakati Dk. Jesca Nkwabi (kulia), akikabidhi cheti cha kuhitimu programu ya Niongoze Fellowship ya mwaka 2021 kwa Mhitimu Barbara Mlata, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ataka mahakama isifungie vyombo vya habari

**Na Jenifer Gilla**

MJUMBE wa Kamati ya Utendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena, amesema vyombo vya sheria kama mahakama, havipaswi kufungwa na sheria ya habari kutoa hukumu yake kulingana na uzito wa kosa alilotenda mwandishi wa habari.

Meena, alisema hayo jana alipozungumza na wakuu wa idara za uandishi wa habari kutoka vyuo vikuu na vyuo vya uandishi wa habari nchini mjini Morogoro katika warsha ya siku tatu kuhusu uandishi wa habari za uchunguzi zinazowahusu watoto.

Warsha hiyo iliwahusisha walimu na wakuu wa idara za uandishi wa habari, ili kuwapa mikakati ya kuwaandaa na kuwa na waandishi wenye uwezo wa kuandika habari za watoto zenye tija kwa jamii.

Alisema, baadhi ya vipengele vya Sheria ya Huduma ya Habari ya Mwaka 2016, vinalazimisha mwandishi atakapobainika kuwa na kosa afungwe si chini ya miaka mitatu.

"Unapoweka sheria ya namna hii maana yake hakimu analazimishwa kumfunga mwandishi hata kama kosa lake halihitaji kifungo. Si kila kosa linahitaji kifungo kwani makosa mengine unaweza kupewa onyo.

"Lakini kwenye sheria hii, hakimu hapaswi kutoa kifungo cha miaka miwili, mmoja au chini ya miezi sita. Pengine mwandishi kafanya kosa linalohitaji kifungo cha mwezi mmoja, kwa mujibu wa sheria hii ni lazima kifungo kianzie miaka mitatu. hili halijakaa sawa," alisema Meena.

aliwaeleza wakuu hao wa idara kwamba mchakato wa mabadiliko hayo ni mawazo ya taasisi nyingi nchini, na kwamba mapendekezo ya habari yamebeba mawazo ya taasisi zote 12 zilizoshiriki katika uandaaji wake.

"Mchakato huu si wa TEF peke yake, ni muunganiko wa taasisi mbalimbali kwa uchache zikiwamo Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN), Baraza la Habari Tanzania (TEF), TWAWEZA na Jamii Forums," alisema Meena.

Aidha, alipendekeza muundo wa vyombo vilivyoelekezwa na sheria iliyopo, kuvunjwa na kuunda chombo kimoja ambacho kitakuwa imara na kusimamiwa kisheria kama ilivyo katika taaluma nyingine nchini.

"Sheria inataja kuwapo kwa Bodi ya Ithibati, Baraza Huru la Vyombo vya Habari pia mfuko wa waandishi. Kuwa na vyombo vyote hivi vinavyofanya kazi ya aina moja, tunasema hapana," alisema.

Pia, alizungumzia hatua ya sheria kumpa mamlaka makubwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari MAELEZO kufungia vyombo vya habari kwa utashi wake.

"Tunasema jambo hili halikukaa vizuri, kumpa mamlaka mtu mmoja kuamua hatma ya kazi za watu sio sawa. Mkurugenzi huyo akifunga chombo maana yake amefunga ajira pia amewanyima haki wasomaji," alisema.

Unlocking Public and Private Finance for the Poor

**CookFund**

**Mradi wa Kuongeza Upatikanaji na Utumiaji wa Nishati Safi na Vifaa Bora vya Kupikia Nchini Tanzania**

**WITO WA MAANDIKO YA KUOMBA UFADHILI**

**Muhtasari**
Mradi wa CookFund, unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), ni Programu wa miaka mitatu (2022 - 2024) unaolenga kuharakisha upatikanaji wa nishati safi na vifaa bora vya kupikia Tanzania Bara, ukilenga mikoa mitano ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mwanza. Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO).

Mradi huu pia ni kipengele muhimu katika Programu ya Umoja wa Ulaya ya 'Mbinu Jumuishi za Kuimarisha Minyororo ya Thamani Endelevu ya njia za kupikia nchini Tanzania' na 'Mfuko wa 11 wa Maendeleo ya Ulaya (EDF)', unaolenga kuchangia juhudi za Tanzania katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa kwa kuongeza idadi ya watu wanaotumia njia bora na endelevu za kupikia, na hatimaye kuboresha mazingira, ajira na fursa za kibiashara. CookFund inatoa msaada wa kiufundi na kifedha, na ufadhili wa kifedha unatoleawa kulingana na matokeo yaliyopatikana na mnufaika wa ufadhili.

**Wito wa Maandiko ya Kuomba Ufadhili**
UNCDF inawakaribisha wafanyabiashara na makampuni zinazojishughulisha na mnyororo wa thamani wa nishati safi na vifaa/teknolojia bora za kupikia katika maeneo ya mijini ya mikoa ya mradi, kuandika na kuomba ufadhili wa kiufundi na kifedha kupitia Programu hii. Kwa maelezo zaidi kuhusu mwongozo, ustahikina vigezo vya maombi tafadhali tembelea tovuti ya mradi ili kupata maelezo zaidi. **https://uncdf.link/CfP-CookFund-Tanzania-SW**

Maombi yote yakamilishwe na kutumwa kupitia fomu maalum ya maombi inayoweza kupakuliwa kutoka katika tofuti ya mradi hapo juu.

**Lugha:** Maombi yote yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Mwisho wa kuwasilisha maombi:** Raundi ya kwanza ya maombi itakuwa wazi kuanzia tarehe 1 Septemba 2022 hadi 16 Desemba 2022.

**Warsha kabla ya uwasilishaji:** UNCDF itaandaa warsha ya nusu siku ili kutoa mwongozo kwa waombaji (watakaopenda) kuhusu wito huu. Lengo ni kutoa fursa kwa waombaji kuuliza maswali na kupata mwongozo zaidi kutoka UNCDF. Ikiwa unataka kushiriki warsha hii, tafadhali tuma barua pepe kwa **cookfund.tz@uncdf.org** yenye kichwa cha habari *"Warsha Kabla ya Uwasilishaji wa Wito wa UNCDF"*. Tafadhali onyesha mkoa unakofanyia kazi zako (*yaani, Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Dodoma na Mwanza*). Tarehe na ukumbi wa warsha utathibitishwa kwa washiriki muda muafaka kwa kila mkoa utakapopangwa. Waombaji watatakiwa kubeba gharama zao wenyewe za kuhudhuria warsha hii.

Tafadhali kumbuka kuwa kuhudhuria katika warshahii sio kati ya masharti/vigezo vya kutuma maombi ya ufadhili.

Kwa habari zaidi na / au maswali, tafadhali wasiliana na:

**UNCDF Tanzania, Barua pepe: cookfund.tz@uncdf.org**
**Tel: +255 22 260 0911**

217022102

# TAMISEMI yatoa mikopo kidigitali

**Na Mary Geofrey**

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeanza rasmi kutumia mfumo wa kielektroniki wa kutoa mikopo ya asilimia 10 inayotokana na makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, wakati akihojiwa kuhusu uanzishwaji wa mfumo huo.

Prof. Shemdoe alisema tayari TAMISEMI imeanza kutumia mfumo wa kutoa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ambayo hukusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa wanawake vijana na wenye ulemavu.

"Kwa sasa vikundi vinaweza kujisajili na kutuma maombi kwa njia ya mtandao," alisema Prof. Shemdoe.

Alifafanua kuwa matumizi ya mfumo huo utatusaidia kuongeza uwazi wa uombaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo.

Alisema kuwa mfumo utasaidia kuongeza uwajibikaji, usawa na uadilifu katika kutoa huduma ya mikopo kwa vikundi husika na kusaidia kuwa na takwimu sahihi na kurahisisha utoaji wa mikopo kwa wakati.

"Kupitia mfumo huu itatusaidia sana kuhakikisha kwamba waombaji wanapata mikopo kwa uwazi lakini pia kuhakikisha zile fedha zinazokopeshwa zinakuwa rahisi sana kurejeshwa,"alisisitiza Prof. Shemdoe.

Prof. Shemdoe alitumia fursa hiyo kuwaelekeza maofisa maendeleo katika halmashauri zote nchini kuhakikisha wanaanza kutoa mikopo kwa kutumia mfumo huo.

"Tunataka Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zote, kuanza kutumia mfumo huu wa kielektroniki ambao tumeanza kuutumia. Na pia ili kujisajili kuomba mikopo tumia anuani hii ya mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz."

Akifafanua zaidi kuhusu utaratibu, Prof. Shemdoe alisema kwanza inaanza kikundi kujisajili kwa kutengeneza akaunti yake na kuweka taarifa sahihi na endapo taarifa zote zitakuwa sahihi mfumo utakutumia barua pepe au ujumbe mfupi kwenye namba ya simu kwa ajili ya uhakiki.

Alisema baada ya utaweza kuingia ndani ya mfumo ili kumalizia kujaza taarifa mbalimbali za kikundi zikiwamo taarifa za wanakikundi pamoja na viambatisho mbalimbali kama katiba na kisha kuziwasilisha taarifa za kikundi kwenye mfumo kwa ajili ya kupata hati ya usajili.

Aidha, alisema baada ya kupata hati ya usajili ambayo inapatikana pia kwa njia ya kielektroniki, kikundi kinaweza kuomba mkopo kwa kuwasilisha maombi yake kwa njia ya mfumo na kupitishwa na kamati mbalimbali za mikopo kwa kuzingatia vigezo vyote.

"Na ili kufanya marejesho hakikisha unapata kumbukumbu ya malipo ya kikundi na lipa kupitia njia yoyote ya malipo," alisema.

# Mchungaji afungwa jela miaka 30 kwa ubakaji

Na Julieth Mkireri, KIBAHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi mkoa wa Pwani imemhukumu kwenda jela miaka 30 mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Chalinze Dayosisi ya Morogoro, Boniface Mgalula baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka na kumpa mimba mwanafunzi.

Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Pwani, Joyce Mushi, alisema Mahakama imemkuta na hatia mtuhumiwa katika makosa mawili yaliyokuwa yakimkabili baada ya kujiridhisha na ushahidi uliotolewa.

Aidha, Hakimu alisema ushahidi uliotolewa mahakamani hapo ni upande wa mlalamikaji na wa kipimo cha vinasaba (DNA) ambacho kilithibitisha kwa asilimia 99.9 kwamba mtoto aliyezaliwa na mwanafunzi huyo ni wa Mchungaji Mgalula.

Alisema kutokana na ushahidi huo mshtakiwa amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela na rufani iko wazi

Waendesha mashtaka wa mahakama hiyo upande wa Jamhuri, Aurelia Makundi na Sofu Bimbiga walidai mahakamani hapo kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo Januari 6, 2020 huko Chalinze, Wilaya ya Bagamoyo.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mchungaji huyo alimbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha tatu mwenye umri wa miaka 16 aliyekuwa akisoma sekondari.

Shauri hilo la jinai namba 57 ya mwaka 2021 kabla ya kufikishwa katika mahakama hiyo lilianza kusikilizwa katika Mahakama ya Mwanzo Lugoba, mkoani Pwani.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro Mkoani Manyara, Dk Suleiman Serera (kulia) na Mbunge wa Simanjiro Christopher Ole Sendeka (kushoto), wakijadiliana na Mkurugenzi wa kampuni ya Franone mining and Gems Ltd, Onesmo Mbise (katikati) baada ya kampuni hiyo kutangazwa kushinda zabuni ya uchimbaji madini ya Tanzanite kitalu C, Mji mdogo wa Mirerani mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: GIFT THADEY**

# Familia yaishangaa polisi kumwachia mtuhumiwa aliyenajisi mtoto darasa 6

Na Gideon Mwakanosya, SONGEA

FAMILIA inayoishi Mjimwema A, imelilalamikia Jeshi la Polisi, mkoani Ruvuma kwa madai ya kumwachia mtuhumiwa wa ubakaji na ulawiti wa mtoto wao aliyekuwa mwanafunzi wa darasa la sita, mwenye umri wa miaka 12.

Wakizungumza na waandishi wa habari mjini hapo, kiongozi wa familia hiyo (jina linahifadhiwa), ameonesha kusikitishwa na kitendo hicho alichokiita kuwa ni cha kinyama na kushangaa jeshi hilo kumwachia mtuhumiwa wa ubakaji na ulawiti.

Alidai, siku ya tukio Agosti 24, majira ya saa 1.30 asubuhi, mama wa mtoto huyo alimtuma watoto wake wawili, akiwamo aliyetendewa kitendo hicho kwenda kununua sukari kwenye duka la jirani.

Inadaiwa walipofika walimkuta mmiliki wa duka hilo, Mustafa Keya, ambaye alimwamuru mmoja wa watoto hao arudi nyumbani na kumwacha dada yake dukani.

Alidai, wakati mtoto huyo anaendelea kusubiri huduma, alishikwa mkono na kuingizwa ndani na muuza duka huyo na kumfanyia kitendo cha kinyama cha kumnajisi huku akimtishia asiseme chochote na akisikia ametoa taarifa kwa mama yake atamuua.

Baada ya unyama huo, imedaiwa mtoto huyo alipewa sukari aliyokwenda kununua na pipi na kurudi nyumbani bila kumwambia mama yake kwa kuogopa vitisho vilivyotolewa na mtuhumiwa.

Hata hivyo, alidai mtoto alipoona maumivu yanazidi alilazimika kumwambia mama yake ambaye baadaye aligundua kuwa mtoto wake hayupo katika hali ya kawaida.

Uongozi wa Serikali ya Mtaa wa Mjimwema na Ofisa Mtendaji, walipewa taarifa na kuchukua jukumu la kutoa taarifa kituo cha polisi na mtoto alikimbizwa hospitali baada ya kupewa fomu ya polisi ya matibabu (PF3).

Askari walifika eneo la tukio na kumkamata muuza duka huyo, lakini walishangaa Agosti 29, mtuhumiwa kuachiwa wakati hali ya mtoto ikiwa mbaya.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Mjimwema A, Halaness Mwabalogile, alikiri kutokea kwa tukio hilo ambalo alidai kuwa ni la kinyama na alishangazwa kuona kuwa mtuhumiwa wa ubakaji na ulawati aliyekuwa mikononi mwa polisi kuachiwa.

Mtendaji wa Kata ya Mjimwema, Stan Kibiki, aliliambia Nipashe kuwa tukio hilo lilitokea kwenye eneo la kata yake na hatua za awali zilishachukuliwa na kufanikisha kumkamata mtuhumiwa, lakini hajaelewa kwanini mtuhumiwa ameachiwa.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Ruvuma, Harison Hussein alipoulizwa kwa njia ya simu kuhusu tuhuma hizo, alisema taarifa hizo ndiyo anazisikia ingawa tukio hilo limetokea zaidi siku tano na kudai kuwa ni mgeni alikuwa hafahamu chochote na kuomba alifanyie kazi kulifuatilia.

## 20 akiwamo diwani mbaroni tuhuma kukutwa na viuatilifu vya mikorosho

Na Hamisi Nasri, MTWARA

JESHI la Polisi mkoani Mtwara linawashikilia watu 20 akiwamo Diwani wa Kata ya Lulindi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Ajali Mpataga kwa tuhuma za kukutwa na viuatilifu vya mikorosho ambavyo ni ruzuku ya serikali kinyume cha sheria.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Mtwara, Aizaki Mushi, watuhumiwa hao wamekamatwa mwishoni mwa wiki kwa nyakati tofauti huku wakiwa wamekutwa na viuatilifu hivyo vya serikali.

Alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), ilifanya uchunguzi wa kufuatilia jinsi viuatilifu hivyo vinavyogawiwa kwa wakulima na kubaini wapo baadhi ya watu wanaohujumu kwa manufaa yao binafsi.

Kamanda Mushi alisema baada ya uchunguzi alifanya upekuzi kwa watuhumiwa hao na kuwakuta na mifuko ya viuatilifu pamoja na dawa za kimiminika ambavyo vyote vilipaswa kutolewa kwa wakulima wa korosho kama ruzuku. Alisema jumla ya viuatilifu ambavyo watuhumiwa hao wamekutwa navyo ni mifuko 148 ya salfa ya unga na dawa za maji chupa 104, zote zilikuwa wapewe wakulima kama serikali ilivyoelekeza.

"Tunawashikilia watu 20 kwa kuwakuta na viuatilifu vya serikali kinyume cha sheria na watuhumiwa hawa wote tutawafikisha mahakamani hivi karibuni kwani wamewakosesha wakulima kupata pembejeo za kilimo," alisema Kamanda Mushi.

Alisema watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani upelelezi utakapokamilika.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa katika wilaya za Newala, Tandahimba na Masasi na kwamba polisi inaendelea na uchunguzi dhidi ya watu wengine ambao pia wamejihusisha na hujuma hizo.

Pia, Jeshi hilo limebaini baadhi ya wafanyabiashara mkoani humo kuwarubuni wakulima wa korosho iwauzie viuatilifu hivyo wanavyopewa na serikali kwa bei ya chini na kuviuza kwa bei ya juu.

Alisema Jeshi hilo litawakamata wafanyabiashara hao na kuwafikisha katika vyombo vya sheria ili sheria ichukue mkondo wake kwa kosa la kuhujumu uchumi.

# 'Wapendeni wafanyakazi wenu wa ndani kuepusha matukio mabaya'

**Na Sabato Kasika**

WAAJIRI wa wasaidizi wa kazi za ndani, wametakiwa kuwaheshimu na kuwafanya marafiki ili kuepuka matukio mabaya kwenye nyumba zao yanayotajwa kusababishwa na wasaidizi hao.

Mkurugenzi wa taasisi isiyo ya kiserikali inayohudumia watoto wa kichwa kikubwa, mgongo wazi na wenye mahitaji maalum ya Kaya Foundation, jijini Dar es Salaam, Annapili Ngome, alitoa rai hiyo juzi.

Annapili alikuwa miongoni mwa washiriki wa semina ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi, iliyoandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, na kusema wafanyakazi hao wana haki sawa na watu wengine.

"Mtu ambaye ana mfanyakazi wa ndani, anatakiwa kuheshimiwa, kumfanya kuwa rafiki ili kuepusha migogoro, kwani una matukio mengi mabaya yanatokea huku wafanyakazi hao wakidaiwa kuwa chanzo," alisema Ngome.

Alitaja baadhi ya haki za mfanyakazi wa ndani kuwa ni kulipwa mshahara, mkataba wa kazi, likizo, kupendwa, kusaidiwa majukumu, kulindwa, kuheshimiwa, kusikilizwa na kuchukuliwa kama mwanafamilia.

"Bahati mbaya, kwenye baadhi ya familia hayo yamekuwa hayafanyiki, hali ambayo ni hatari, hivyo wito wangu ni kwamba tuwatimizie mahitaji yao na kutowabagua, kwani nao wana haki," alisema.

Alisema katika baadhi ya familia, mfanyakazi wa ndani anatengwa mbali wakati wa chakula na pia analazwa sehemu mbaya, kudharauliwa na watoto wa bosi wake, hali inayoongeza chuki.

"Sio vibaya bosi unaponunulia watoto wako nguo, mnunulie pia, ukitoka na familia yako, ambatana naye, unapokula na watoto wako mezani naye awepo, pia mfundishe mambo mengi kuhusu maisha," alisema.

Mweka hazina wa taasisi inayojishughulisha na uwezeshaji wa wanawake kijamii na kiuchumi ya Nyota TZ, Mwanakombo Ramadhan, alisema wafanyakazi wa ndani ni watu muhimu na faida katika familia.

Iwapo mfanyakazi wa ndani hatabaguliwa, atakuwa wazi kukushirikisha mambo ambayo hata wazazi au marafiki zake hajawahi kuwaambia, atafanya kazi zote kwa moyo wa kupenda na uhiyari," alisema Mwanakombo.

Vile vile, atakuwa anajituma kufanya mambo ambayo sio kazi zake kwa sababu anajua anamsaidia rafiki yake, na kwamba kuna ujuzi ambao unao utaanza kuambukizwa ndani yake.

"Maono, tabia na shauku ulivyonavyo vitaanza kuambukizwa ndani yake na atajiona anawajibu wa moja kwa moja wa kukuunga mkono, pia atawatumikia watoto wako hata kama haupo watoto hawataona kupungukiwa, kwani ataishi nao kwa upendo wa hali ya juu," alisema.

Kwa njia hiyo, mfanyakazi atamjali na kujua nini bosi wake anapenda na atamtendea mema, ataona ana wajibu wa moja kwa moja wa kulinda na kutunza mali za bosi wake.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii, Seleman Bishagazi alisema, wamefanya semina hiyo kwa lengo la kutaka kuhakikisha wanawake na wasichana wanaondokana na unyanyaji na ukatili wa kijinsia.

"Kituo chetu kimepata ufadhali kutoka Women Fund, ili kuendesha semina kwa ajili kuwajengea uwezo wanawake na wasichana waweze kuondokana na vikwazo vya kiuchumi, kijamii na hata kisiasa," alisema Bishagazi.



Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa David Msuya ambaye pia ni mshauri na mwanahisa wa benki ya Mwanga Hakika, akizungumza katika mkutano mkuu wa pili na wanahisa wa benki hiyo, wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro juzi. Kulia ni Mjumbe wa bodi ya benki hiyo, Zukra Ally. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi/walezi wanaotelekeza watoto vituoni waonywa

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

WAZAZI na walezi wameonywa tabia ya kutelekeza watoto vituoni na kusababisha mzigo wa malezi kwenye vituo vinavyopokea watoto hao.

Onyo hilo limetolewa na Kituo cha Ntoma, Halmashauri ya Bukoka mkoani Kagera, kinachomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheli Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Magharibi (DKMG).

Tangu kilipoanzishwa miaka 70 iliyopita, hupokea watoto waliofiwa na wazazi wao wakati wa kujifungua na wanaotelekezwa na mama zao baada ya kuzaliwa na kuokotwa mitaani.

Akizungumza wakati wa harambee ya kuchangia matunzo ya watoto hao, Mkuu wa kituo cha Ntoma, St. Penina Kaimukirwa alisema kuwa, kituo hicho kinapokea watoto wenye umri wa kuanzia mwaka sifuri hadi miwili, na mtoto anapozidi umri huo hupaswa kuchukuliwa na wazazi au walezi ili akalelewe katika familia.

Kama hawana wazazi au walezi hupaswa kupelekwa katika vituo vinavyolea watoto wakubwa, lakini imebainika kuwa wakishapelekwa kwenye vituo hivyo hawarudi kuwasalimia watoto wao.

"Wazazi wengine wakishaleta watoto wao hapa wanawakwepa, wakati siku ya kuwaleta wanakuja wananyenyekea na kubembeleza ili mtoto apokewe, lakini akishapokewa wakiondoka hata hawageuki nyuma, na tukifuatilia kwa kushirikiana na idara ya ustawi wa jamii kupitia serikali za maeneo walipoandikisha wametoka, utaambiwa huyu mtu alikwishaondoka akaenda visiwani au alikuwa mpangaji hatujui alihamia wapi," alisema St. Kaimukirwa.

Mchungaji kutoka KKKT DKMG, Dk. Elimeleck Kigembe, alisema kutokana kituo hicho kutelekezewa watoto na wazazi au walezi, wakati mwingine wanatafuta vibali ustawi wa jamii ili polisi wawasaidie kuwatafuta.

Mkuu wa dawati la jinsia na watoto katika wilaya ya Bukoba, Betrida Minga, alisema chanzo kikuu cha watoto kutelekezwa mitaani ni migogoro ya kifamilia na wazazi wanapogombana na kushindwa kuelewana, mama anakasirika na kutupa mtoto.

Mbunge wa Bukoba Vijijini, Dk. Jason Rweikiza aliyeshiriki harambee hiyo, aliwaomba wananchi na wadau wengine kujitolea kuwachangia watoto hao ili wapate mahitaji yao ya kila siku.

Katika harambee hiyo zaidi ya Sh. milioni 30 zilipatikana, ambazo zitatumika kwa ajili ya kuwanunulia maziwa watoto 33 walioko katika kituo hicho, kwa muda wa mwaka mmoja.

# Benki zashauriwa kutowasahau wateja wadogo

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Clepa Msuya ameishauri benki ya Mwanga Hakika kuwahudumia wateja wadogo ambao ndiyo lengo kuu la kuanzishwa kwa benki za kijamii nchini.

Msuya ambaye ni mwanahisa wa benki hiyo alitoa ushauri huo juzi Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro, wakati akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa pili wa wanahisa wa benki hiyo.

"Nipende kuomba benki hii iendelee na mchakato wa kuwa benki kubwa ya biashara na isisahau kuhudumia wateja wadogo wadogo ambao ndiyo walikuwa lengo kuu la kuanzishwa kwa benki hizi za kijamii," alisema.

Msuya alitoa historia fupi ya kuanzishwa Mwanga Community Bank na kusema ilikuwa na lengo la kuwa benki ya jamii.

Alimpongeza Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Ridhiwan Mringo na bodi yake kwa kazi kubwa waliyoifanya na aliwaomba waendelee na kazi nzuri ambayo waliianzisha huku akiwataka wanahisa watafakari namna benki hiyo inavyowasaidia.

Naye mwakilishi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Leodgar Haule, aliipongeza benki hiyo kwa kufanya vizuri kwa kipindi cha muda mfupi na aliipongeza kwa mtaji ambao imepata hadi kufikia hatua ya kuwa benki ya biashara.

"Nawapongeza wote hasa uongozi wa Benki ya Mwanga Hakika pamoja na wanahisa wote kwa juhudi mzifanyazo kuhakikisha inapata maendeleo zaidi, pia niiombe benki hii iendelee kufanya kazi kwa bidii na kufuata sheria mbalimbali zilizopo," alisema.

Alisema, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kusimamia na kutoa ushauri kwa kuwa ni msimamizi mkuu wa benki nchini.

Mkutano huo ulikuwa na lengo la kuimarisha uhusiano uliopo baina ya wanahisa hao na benki hiyo, ili kuwataarifu wanahisa hao kuhusu benki hiyo ilipotoka, ilipo na pia inapokwenda ili kupata taarifa kamili na ili wanahisa hao waweze kutathmini maendeleo ya benki hiyo na kubaini changamoto ili ziweze kutatuliwa.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wanahisa zaidi ya 300, wakiwamo waasisi na viongozi mbalimbali wa benki hiyo na Mhandisi Ridhiwani Mringo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi.

NI ZAMU YA MGOMBEA HURU
LHRC wakumbushia hukumu kesi ya Mtikila, watamani serikali imruhusu Ukurasa 13



Ukurasa 14



## Uchaguzi Angola; UNITA yaanguka kishujaa kwa MPLA, ikisomba 62% kura jijini Luanda



FAHAMU CHIMBUKO LA UWANJA JOHN MWAKANGALE

# Jina la penye maonyesho kilimo kumuenzi mkongwe wa Mbeya

- Kipenzi mkoa, Nyerere aliyemkaribisha Mandela 1962
- RC mstaafu Paul Kimiti asimulia walivyolikokotoa jina

**NA MWANDISHI WETU**



Mwalimu Julius Nyerere (kulia) akipokea zawadi iliyoandaliwa na wanawake siku ya Maonyesho ya Sabasaba ambayo yalikuwa maalumu kwa wakulima, Julai 7, mwaka 1978, kulia kwake ni John Mwakangale. **PICHA: JBM MAKTABA**

HIVI sasa mtu anapofika katika jiji la Mbeya na hasa anayetokea barabara ama itokayo Iringa hadi jijini Dar es Salaam, au makutano barabara itokayo Tukuyu, Kyela hadi Malawi, ni lazima anakutana na Viwanja vya Maonyesho vya John Mwakangale.

Ni viwanja vyenye unasababa wa moja kwa moja na uzalishaji wa kilimo. Lakini, bado kunabaki swali, huyo Joh Mwakangale ni nani? Hapo ndipo kimkoa ana unasaba na mengi, akiwa sehemu muhimu ya maendeleo mkoa, pia siasa zake.

Marehemu Mwakangale amedumu maisha yote, akiwa swahiba wa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, akiwa na la ziada, kwani hata mwanasiasa mwanadamizi wa Afrika Kusini, Nelson Mandela alipofika nchini kwa mara ya kwanza mwaka 1962, aliyempokea jijini Mbeya kwa niaba ya Nyerere, alikuwa Mzee Mwakangale.

Wakati Mwalimu Nyerere na swabiba wake, Mzee Mwakangale, mzaliwa wa kijijini Suma, Tukuyu wilayani Rungwe, akadumu katika falsafa 'Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa', akibuni Maonyesho ya Kilimo ya Nanenane, akilenga kukuza chachu kilimo kwa wakulima kitaifa, akisitiza ukuzaji kilimo kwa wananchi na umma wa Watanzania kujihakikishia usalama wa chakula.

Mwalimu Nyerere, akisaidiana na timu yake ya uongozi, akiwemo Mwakangale, yuko katika walioonesha jitihada za chama tawala (TANU na baadaye CCM) na kiserikali kuifikia falsafa 'Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa,' huku katikia Azimio la Arusha, pia

Hapo ikaendana na mikakati ya kuondokana na maadui wakuu watatu kitaifa; Ujinga, Maradhi na Umaskini. Tena, hukosi kumtaja John Benedict Mugogo Mwakangale, maarufu JBM), hasa upande wa Nyanda za Juu Kusini.

Leo hii, marehemu Mwakangale, ni miongoni mwa wanasiasa maarufu ambaye kwa sasa kumbukumbu yake inasalia kwenye maandiko tofauti, mkoa wa Mbeya ukimpa kumbukumbu maalumu Uwanja Uwanja wa Maonyesho ya Nanenane wa John Mwakangale, iliyopo eneo la Uyole, Mbeya.

Maonyesho ya Nanenane ambayo mwaka huu yamefanyika kitaifa jijini humo, mgeni rasmi akiwa Rais Samia Suluhu Hassan, yamekutanisha wadau wengi wa kilimo zikiwamo taasisi, wakulima, utafiti kutoka mikoa inayounda Nyanda za Juu Kusini, maarufuku kwa jina 'The Big Four.'

Hiyo, ni mikoa minne; Iringa, Ruvuma, Rukwa na Mbeya. inayotikisa kitaifa katika kuzalisha vyakula na hasa nafaka.

**RC MSTAAFU PAUL KIMITI**

Paul Kimiti, aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya miaka ya 1990, anaiambia Nipashe kwamba wakati inaamuliwa kuwapo eneo maalum kwa ajili ya maonyesho hayo, mapendekezo yakaendana na hoja iwe kituo kipindi hicho. Kimiti anaendelea:

"Tuliona Uyole eneo kuliko na kituo cha Kilimo, panafaa kwa ajili ya maonyesho na kwa kuwa John Mwakangale alikuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, nilimshirikisha kwamba tuwe na kituo hiki. Nilimuomba tutie nguvu pamoja na pia kujenga heshima ya mkoa."

Anaeleza, kabla ya kamati iliyoteuliwa kupitisha jina moja kati ya mengi yaliyowasilishwa, kikao kilifikia uamuzi wa jina la John Mwakangale, liwe rasmi kwa ajili ya uwanja huo.

Hapo Chama cha Kilimo Tanzania (TASO), kilipoandaa maonyesho kikanda mahali hapo kikashirikisha mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma. (sasa kuna mikoa ya ziada; Njombe, Katavi na Songwe) waamue kuyaweka kikanda mjini Mbeya kikanda.

"Mkutano ukapendekeza majina mengi, ila Mkuu wa Mkoa wa wakati huo alipendekeza jina la John Mwakangale, kwanza akisema alikuwa mbunge wa Nyanda za Juu Kusini kwa muda mrefu na harakati nyingi za kitaifa, kimataifa na mkoa, apewe heshima hiyo," anasema.

**HISTORIA YA NANENANE**

Historia ya maonyesho hayo ni tangu kupatikana Uhuru, yakifanyika katika ngazi za wilaya na mikoa, ukiwamo mfano wa 'Nyamwezi Agricultural Show' yaliyofanyika katika miaka ya 1949 hadi 1950, katika mikoa ya Kanda ya Ziwa; Mwanza, Tabora na Shinyanga, wakulima na wafugaji wakionyesha bidhaa zao.

Baada ya Uhuru mwaka 1961, shughuli ya Maonyesho ya Kilimo na Sherehe za Wakulima, viliendelea kuwapo na baadaye kujulikana kama Maonyesho ya Sabasaba.

Katika kipindi cha maonyesho ya Sabasaba (wakati huo) mapungufu mengi yaliyojitokeza ni pamoja na kushindwa kufikisha teknolojia mbalimbali za kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima na wadau wengine ipasavyo na pia maonyesho yalikuwa na sura ya kutoa zawadi tu kwa washindi bora wa vijiji, wilaya, taasisi na mashirika ya umma.

Mnamo Oktoba 20 mwaka 1992, Wizara ya Kilimo iliitisha kikao

INAENDELEA UK.12

# Ushindi wa Ruto sasa wakataliwa kila kona wengine tisa waungana na Raila

**Na Mwandishi Wetu**

RUTO anapingwa kila kona pengine ndivyo wanavyoweza kusema wanaofuatilia matokeo ya uchaguzi wa Kenya, kufuatia kesi zilizofikishwa kwenye mahakama ya juu kuhoji uhalali wa ushindi wa Rais Mteule William Ruto.

Wakati mgombea wa Azimio la Umoja, Raila Odinga, na mgombea mwenza wake, Martha Karua, makundi mbalimbali ya ndani na nje ya nchi yamejiunga na Raila na Martha, kufungua kesi mahakamani kupinga ushindi wa Makamu Ruto.

Raila na mgombea mwenza wanasubiri mahakama ya juu, kuamua hatima yao, baada ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo (IEBC), kumtangaza Makamu Ruto kuwa mshindi.

Kwa upande wake , Raila anachotaka ni kupata haki yake kwa maelezo kuwa uchaguzi huo ulijaa udanganyifu na kumpendelea Rais Mteule Ruto.

Azimio la Umoja wanadai, pamoja na mambo mengine, Ruto hakujinyakulia asilimia 50, pamoja na kura moja iliyohitajika ili mgombea huyo kutangazwa mshindi wa uraia na kwamba Mwenyekiti wa IEBC, Wafula Chebukati, alitangaza matokeo bila kujumlisha na kuhakiki kutoka maeneo bunge 27, ambayo yangefanya uchaguzi hali iliyoathiri hesabu ya mwisho.

Wawili hao zaidi wanasema, tume haikuhesabu kura 250,000 ambazo zilipigwa bila kujumuisha kura zilizopigwa na wapigakura waliopigakura wenyewe. Mahakama ya juu zaidi imekubali maombi mengine manane ya uchaguzi wa urais, tofuati na ya kando ya Odinga na Karua huku sita kati yao yakipinga ushindi wa Ruto.

Aidha, upande Raila unataka ufanyike ukaguzi wa kisayansi ya 'forinsik' kwenye vifaa, mfumo na teknolojia zote zinazotumiwa na IEBC katika uchaguzi wa urais na Chebukati kutangazwa kuwa si mtu sahihi kushikilia ofisi ya umma.

Wale wanaopinga ushindi wa Ruto wakiongozwa na Odinga na wanachama wa mashirika ya kiraia wameibua madai mbalimbali kwamba hesabu hiyo ilihusisha "uhalifu," "udanganyifu" na umezungukwa na makosa mengi ya kiuchaguzi.

Pamoja na Odinga na Martha Ruto anapingwa na John Njoroge Kamau, wanaharakati wanne wakiongozwa na Khelef Khalif, Youth Advocacy Africa na Peter Kirika, David Kariuki Ngari, Seneta wa Busia Okiya Omtatah na raia wengine Juliah Nyokabi Chege na wengine wawili.



Jaji Mkuu wa Kenya Martha Koome, anatarajiwa kuongoza majaji kwenye kesi ya kupinga ushindi wa Ruto.



William Ruto, Rais Mteule wa Kenya anayevaa tabasamu muda wote licha ya mpinzani wake Raila Odinga, kutinga kortini.
**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Ombi lingine liliwasilishwa na Reuben Kigame, ambaye alijaribu kugombea lakini alifungiwa nje ya kinyang'anyiro hicho na IEBC.

### DIASPORA YAMPINGA

Kwa kuunga mkono hatua ya kupinga ushindi wa Ruto, Seneta wa Busia Okiya Omtatah, na wengine hawakubaliani na matokeo ya uchaguzi wa urais kwa msingi kwamba hakuna hata mmoja wa wagombea wanne wa urais William Ruto, Raila Odinga, George Wajackoya na Waihiga Mwaure aliyepata asilimia 50 pamoja na kura moja kama inavyotakiwa na katiba.

Anasema uchambuzi unaonyesha kuwa hakuna mgombea aliyepata asilimia 50 pamoja na kura moja kama inavyotakiwa na katiba kwa sababu tume ya uchaguzi haikuzingatia kura ambazo hazijahesabiwa za watu waliopigakura kwa mikono siku ya uchaguzi (kwenye makaratasi).

Mwanaharakati huyo anaongeza kuwa hakuna sheria inayompa mamlaka Mwenyekiti wa wa IEBC kutangaza mgombea yeyote kuwa rais aliyechaguliwa kihalali na kwamba hakuzingatia wapigakura waliopigakura wenyewe, ambao jumla yao ni 140,028.

Aidha, anaitaka mahakama kufuta matokeo ya uchaguzi wa urais yaliyotangazwa na mwenyekiti huyo wa IEBC.

Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Masuala ya Diaspora wa Kenya John Maina, anaungana na Omtatah kumpinga Ruto akiwa pamoja na Nyakina Wyclife Gisebe na Victor Okuna.

Wengine wanaompinga Ruto ni Khelef Khalifa, anayedai kuwa uchaguzi wa urais uliokamilika uliendeshwa vibaya, ulisimamiwa na kutangazwa na IEBC bila kufuata vigezo.

Kwa pamoja na walalamikaji wengine George Osewe, Ruth Mumbi na Grace Kamau, pia wanadai mwenyekiti Chebukati alikosea pale alipowatenga makamishna wengine akiwamo Naibu Mwenyekiti Juliana Cherera, Francis Wanderi, Irene Masit na Justus Nyang'aya, Abdi Guliye na Boya Molu.

Wanasema kuwa, Chebukati alipaswa kuwahusisha makamishna wote na kwamba kutengwa kwao kunafanya tamko lililotolewa na mwenyekiti huyo wa IEBC kuwa kinyume cha sheria.

### 700,000 WALIEUNGULIWA

Raia mwingine anayejitambulisha kama mpigakura anayewasilisha ombi hilo pamoja na wapiga kura wengine wawili, Joseph Mutua Ndonga na Simon Mwaura Njenga wanasema , tume ya uchaguzi ilikiuka sheria za uchaguzi katika muda wa uchaguzi mkuu na wa urais.

Raia hao wakiwakilishwa na Wakili Kibe Mungai, wanadai kuwa zaidi ya watu 700,000 walienguliwa kinyume cha sheria kwa kushindwa na tume kutoa utaratibu wa kupiga kura chini ya Kanuni Maalum za Upigaji Kura iliyopo kisheria.

Wanadai kuwa, IEBC ilikiuka kanuni za kupigakura kuhusu mahitaji maalum, madai yao mahakamani yanaonyesha kuwa kutokana na madai ya kushindwa, angalau wananchi 500,000 walio chini ya kundi lililohitaji kupiga kura kwa kanuni maalumu, walinyimwa haki yao ya kuchagua.

Aidha, wanahoji inakuwaje askari 180,000 wa vikosi vya usalama walikuwa wakishiriki kulinda uchaguzi, huo wasipige kura? Kwanini hawakuweza kupiga kura na kupuuzwa haki yao ya kuchagua viongozi?

Wanadai kuwa teknolojia iliyotumwa na tume haikuwa wazi, isiyowajibika na haikuwa wazi hivyo matokeo si halali.

Katika uchaguzi huo Muungano wa Kenya Kwanza unaoongozwa na Naibu Rais William Ruto, umepata wabunge 159 katika Bunge la Kitaifa huku Azimio la Umoja-One Kenya inayoongozwa na Waziri Mkuu wa zamani Raila Odinga ina wabunge 162 zaidi kuliko chama kilichoshinda.

***MITANDAO***

# Jina la penye maonyesho kilimo kumuenzi mkongwe wa Mbeya

**INATOKA UK.11**

mkoani Arusha na ikaridhiwa kuanzishwa kwa Chama cha Kilimo Tanzania (Tanzania Agricultural Society Organisation -TASO) maalum kwa ajili ya kuratibu Maonyesho ya Kilimo. Iliandikishwa rasmi mwaka 1993.

Wizara ya Kilimo, Mifugo na Ushirika, ilisimamia kuanzishwa chombo hicho cha Serikali na kikapewa jukumu la kuratibu na kuendesha Maonyesho na Mashindano ya Kilimo.

TASO, iliratibu maonyesho ya kilimo yaliyofanyika kitaifa nkoani Mbeya kwenye Uwanja wa Uyole, ambao kwa sasa ndiyo unaitwa Uwanja wa Maonyesho ya Kilimo wa John Mwakangale.

Vilevile, mwaka 1994, TASO iliratibu Maonesho ya Pili ya Kilimo yaliyofanyika Kitaifa mjini Morogoro kwenye Uwanja wa Tungi, ambao kwa sasa unaitwa Uwanja wa Maonyesho ya Kilimo wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

TASO, kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo, Mifugo na wadau wengine waliratibu Maonyesho ya Kilimo Kitaifa katika viwanja vya Maonyesho ya Kilimo vya Kikanda ambavyo ni: Themi mkoani Arusha; Mwalimu J.K.Nyerere -Morogoro; John Mwakangale-Mbeya; Nzuguni- Dodoma na Ngongo mkoa wa Lindi.

Viwanja hivyo vilianzishwa kwa lengo la kuwa na Uwanja wa Maonyesho ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika kila Kanda kitaifa, yaliyofanyika kuanzia Agosti Mosi na kufikia kilele tarehe 8 ya kila mwaka.

Kwenye maonesho hayo, wakulima na wadau wengine walipata fursa ya kuonyesha, kujifunza teknolojia mbalimbali za uzalishaji na usindikaji wa mazao, mifugo na uvuvi.

Washiriki walishindanishwa na kupata washindi kulingana na makundi ya bidhaa na teknolojia zao walizozionyesha na TASO ilitoa zawadi kwa washindi mbalimbali ambazo ni; hati, ngao, zana za kilimo, pembejeo na fedha taslimu.

DAI LA MGOMBEA HURU

# LHRC wakumbushia hukumu kesi ya Mtikila, watamani serikali imruhusu

**Na Sabato Kasika**

SAFARI ya muda mrefu ya kusaka fursa ya kuwa na mgombea binafsi katika uchaguzi wa viongozi iliyoanzishwa na mwanasiasa Mchungaji Christopher Mtikila (sasa ni marehemu), inaanza kupata nguvu mpya baada ya baadhi ya mawakili kuibuka na namna bora ya kumrejesha mgombea huru.

Hatua hiyo inatokana na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu LHRC kupendekeza mambo saba kwa serikali, huku namba moja likiwa ni kutekelezwa kwa uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, iliyotoa maelekezo ya kuruhusu kuwapo mgombea huru katika uchaguzi wowote wa kisiasa unaofanyika.

Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Wakili Anna Henga, anasema hayo, katika mkutano wake na wanahabari jijini Dar es Salaam wiki iliyopita katika uzinduzi wa Mwezi wa Demokrasia, kuelekea Siku ya Demokrasia Dunia itakayofikia kilele chake Septemba 15 mwaka huu.

"Tulishirikiana na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na Mchungaji Mtikila dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tulifungua shauri la pamoja Namba 9 na 11 mwaka 2011 kuhusu kuwapo mgombea huru," anasema.



Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) Anna Henga (kushoto), alipozungumzia uwapo wa mgombea huru. **PICHA: SABATO KASIKA**

Anafafanua kuwa mgombea huyo huru ni katika uchaguzi wa kisiasa, ambapo walifungua shauri katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, na kukubaliwa, na kwamba hadi leo serikali haijatekeleza hilo.

"Tunadhani sasa ni wakati muafaka wa kuwa na mgombea huru ili wale ambao hawako katika vyama vya siasa nao waweze kuwatumikia wananchi badala ya kutegemea wagombea kupitia vyama tu," anasema Henga.

Henga anasema kuruhusu mgombea huru kunaweza kuimarisha ustawi wa demokrasia ya vyama vingi nchini, kwa kuwaacha watu kuchaguliwa bila kubanwa na mfumo wa kupitia katika vyama.

Mkurugenzi Mtendaji huyo anataja mapendekezo mengine ya kituo chake kuwa ni kuitaka serikali kutekeleza uamuzi wa Mahakama ya Afrika Mashariki kwenye vifungu vya sheria ya vyama vilivyoamuliwa kuwa vinakinzana na mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Tunapendekeza kuridhia Mkataba wa Afrika wa Demokrasia na Uchaguzi wa 2007, pia kuifanyia marejeo Sheria ya Haki za Msingi na wajibu wa kisheria (The Basic Rights and Duties Enforcement Act)," anasema.

Anataja pendekezo lao lingine kuwa ni kuruhusu wananchi na wadau mbalimbali kuendelea kufanya mijadala, makongamano na midahalo juu ya haki za kidemokrasia na pia Watanzania wapewe katiba mpya kabla ya mwaka 2025 kwa madai kwamba, katiba mpya ni sasa.

Aidha anasema katika kuelekea Siku ya Demokrasia Dunia itakayofikia kilele chake Septemba 15 mwaka huu, kituo hicho kitafanya shughuli mbalimbali ikiwamo utoaji elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuwa na katiba mpya.

"Tutatoa elimu kuhusu umuhimu wa wananchi katika haki za kidemokrasia, mjadala wa haki za kidemokrasia, tathmini ya miaka 30 ya siasa za ushindani nchini na mambo mengine muhimu," anasema.

Aidha, alisema kituo hicho kimekuwa na mc hango mkubwa katika kukuza na kuimarisha haki za kidemokrasia nchini tangu kuasisiwa kwake mwaka 1995, ikiwa ni pamoja na kufungua mashauri mbalimbali yenye maslahi kwa umma, katika mahakama za ndani kikanda na zile za kimataifa.

Anasema takriban miaka 27 tangu kuanzishwa kwa kituo hicho, na kwamba kimekuwa mstari wa mbele kutetea, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu nchini kwa kufungua mashauri mbalimbali yenye maslahi kwa umma.

"Tumefanya hivyo kwa mujibu wa ibara ya 26 na ibara ya 30 (5) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, tunapoona kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za kidemokrasia kinyume na katiba," anasema.

Anafafanua kuwa katika ibara ya 26- (1), inasema kuwa kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

> "Tumefanya hivyo kwa mujibu wa ibara ya 26 na ibara ya 30 (5) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, tunapoona kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za kidemokrasia kinyume na katiba," anasema.

"Ibara ya 30-(1) inasema; Haki na uhuru wa binadamu ambavyo misingi yake imeorodheshwa katika Katiba hii havitatumiwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma," akariri Katiba.

Anatolea mfano ni kesi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali shauri namba 77 la mwaka 2005, katika Mahakama Kuu ya Tanzania Masijala Kuu ya Dar es Salaam, msingi mkuu wa kesi hiyo ukiwa ni sheria ya uchaguzi.

"Hatua hiyo ilitokana na kuruhusu wagombea wa nafasi mbalimnbali za kisiasa kuruhusiwa kutoa 'takrima' kwa wapigaakura, kitu ambacho ni rushwa ambapo mahakama ilikubaliana na waleta maombi kwa kusema takrima ni rushwa na sheria ilirekebishwa baada ya uamuzi huo," anasema.

**SIKU YA DEMOKRASIA**

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC anafafanua, katika kuelekea Siku ya Demokrasia Dunia itakayofikia kilele chake Septemba 15 mwaka huu, kituo hicho kinaendelea na shughuli mbalimbali ikiwamo utoaji elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuwa na Katiba Mpya.

"Ikumbukwe kuwa katika utawala wowote wa kidemokrasia, katiba ni msingi mkuu wa kila kitu. Hivyo miongoni mwa shughuli tunazoshiriki katika mwezi huu wa demokrasia ni pamoja na utoaji wa elimu juu ya umuhimu wa kuwa na katiba mpya," anasema.

Anasema kituo kimeandaa dodoso maalum la maswali mahususi yanayolenga kujua ni lini Watanzania wangependa mchakato wa katiba mpya umalizike, wangependa mchakato huo uanzie wapi.

"Lakini pia tunataka tathmini juu ya uelewa wa Watanzania kuhusu masuala yahusuyo upatikanaji wa katiba mpya.Hadi sasa Watanzania zaidi 1000 wameshiriki kujaza dodoso hilo," anasema.

"Anaongeza kussema; 'Tunatoa elimu kuhusu umuhimu wa wananchi katika haki za kidemokrasia, mjadala wa haki za kidemokrasia, tathmini ya miaka 30 ya siasa za ushindani nchini na mambo mengine muhimu."

Henga anasema kituo hicho kimekuwa na mchango mkubwa katika kukuza na kuimarisha haki za kidemokrasia nchini tangu kuasisiwa kwake mwaka 1995, ikiwa ni pamoja na kufungua mashauri mbalimbali yenye maslahi kwa umma, katika mahakama za ndani kikanda na zile za kimataifa.

# Uchaguzi Angola; UNITA yaanguka kishujaa kwa MPLA, ikisomba 62% kura jijini Luanda

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

BAADA ya majirani Kenya kumaliza uchaguzi wao Agosti 9, na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Majimbo (IEBC), kumtangaza William Ruto, kuwa ndiye Rais Mteule wa Kenya,kadhalika nchini Angola mwanachama wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Kusini mwa Afrika (SADC), wamefanya uchaguzi mkuu.

Ilikuwa ni Agosti 25, Alhamisi iliyopita Tume ya Uchaguzi ya Angola ikitangaza kuwa chama tawala cha MPLA, kilikuwa kinaongoza kukiacha nyuma UNITA, licha ya kwamba watu wengi wanadaiwa kukichoka chama hicho kikongwe barani Afrika kilichotawala kwa karibu miaka 50 sasa.

Kwa maelezo ya tume, chama tawala kimeshinda miaka mingine mitano madarakani kikijizolea asilimia 51, ya kura dhidi ya UNITA iliyopata asilimia 44.95. Hata hivyo ushindi huo unatajwa kuwa ni wa kura zilizopungua na si wa kishindo.

Chama hicho kilishinda kwa kishindo kwenye majimbo ya Luanda kwa asilimia 62 licha ya kwamba idadi yake haikutajwa.

Uchaguzi huo uliofanyika Agosti 24, uliwaweka kwenye ushindani mkali Chama cha People's Movement for the Liberation of Angola'-MPLA' na wapinzani wakuu kutoka chama kilichoasisiwa na Jonas Savimbi, cha 'National Union for the Total Independence of Angola' -UNITA,

MPLA, imeshikilia mamlaka nchini Angola kwa takriban miongo mitano, mingi ikiwa chini ya Rais Jose Eduardo dos Santos, ambaye alikuwa madarakani kuanzia 1979 hadi 2017 alipostaafu na kumuweka mrithi wake Rais João Lourenço.

Katika uchaguzi huo wapinzani UNITA, walikuwa na matumaini ya ushindi wakiamini kuwa wangenufaika kutokana na vijana wa Angola kuchanganyikiwa kutokana na umaskini wanaodhani ni matokeo ya uongozi wa MPLA.

Lakini, mambo hayakuwa hivyo chama tawala kimepata ushindi japo si mkubwa katika uchaguzi huo baada ya tume ya uchaguzi kutangaza kuwa kura zake zimefikia asilimia 51, lakini kiongozi wa muungano mkuu wa upinzani alikataa matokeo hayo.

MPLA, chini ya Rais Lourenço, ilichukua asilimia 51.2 katika uchaguzi wa wiki iliyopita. Mpinzani wake wa karibu, UNITA, alikuwa na matokeo bora zaidi kwa asilimia 44.95

UNITA hapo awali ilisema inatarajia kupinga matokeo.

MPLA, iliyo madarakani kwa takriban miongo mitano, imekabiliwa na ukosoaji juu ya viwango vya juu vya umaskini na ukosefu wa ajira.

Katika uchaguzi huo wapigakura wachache zaidi ya nusu ya waliojiandikisha walijitokeza kwenye uchaguzi wa Jumatano, ambao unaonekana kuwa unaelekea kumpa ushindi Rais Joao Lourenco, muhula wa pili wa miaka mitano na kuongeza utawala unazikubali sera za 'Marxist' na mrengo wa kikomonisti.

Huku zaidi ya asilimia 97, ya kura zikiwa zimehesabiwa, tume ya uchaguzi inasema MPLA ilikuwa mbele kwa asilimia 51 huku mpinzani wake wa muda mrefu, UNITA, akiwa na asilimia 44.95.

Kuanzia hapo tambo zikianza "Tumewafikia watu wengi zaidi. Tuna wanachi wengi wanaotuunga mkono na tutawala bila aina yoyote ya tatizo na tutafanya hivyo," msemaji wa MPLA Rui Falcao, anaawambia wanahabari katika mji mkuu Luanda, jiji ambalo lilipigia kura kwa wingi kwa wapinzani wa UNITA.

Hata hivyo, kiongozi wa UNITA Costa Junior, akihutubia waandishi wa habari na wafuasi wake kwa mara ya kwanza tangu kupiga kura, alikataa kile alichokiita tofauti za "kinyama" kati ya hesabu za tume ya uchaguzi na zile UNITA ilizojumlisha yenyewe.

"Hakuna shaka hata kidogo kwamba MPLA haikushinda uchaguzi," anasema Junior kwa hiyo, "UNITA haitambui matokeo ya awali." Na kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuchunguza hesabu hiyo.

Kuna hofu kwamba mzozo wowote unaweza kuchochea ghasia na Junior, aliwataka Waangola watulie.

MPLA na UNITA, ambazo zamani zilikuwa vikundi vya waasi wanaopinga ukoloni wa Wareno, walikuwa kwenye pande zinazopingana za vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyokuwa vikiendelea baada ya uhuru vilivyodumu hadi 2002 pale kiongozi wa UNITA Jonas Savimbi, alipouliwa kwa kupigwa risasa akiwa porini .

Ikiwa matokeo yatabakia kama kama yalivyo UNITA, kwa mara ya kwanza, itakuwa imeinyima MPLA theluthi mbili ya kura zinazohitajika kupitisha mageuzi makubwa nchini humo kwa kuwa itakuwa na wabunge wengi.

Rais Joao Manuel Lourenço (68), ameahidi kuongeza mageuzi katika muhula wake wa pili, ikiwa ni pamoja na kubinafsisha mali ya serikali zinazoendeshwa bila tija.

Wakati wa uchaguzi UNITA, ilichapisha kibonzo cha mgombea wao Junior kwenye akaunti yake rasmi ya Instagram ikiwa na nukuu: "Rais". MPLA nayo iliweka video kwenye mtandao wa kijamii ya Lourenço akiwashukuru Waangola kwa matokeo ya uchaguzi.

*MITANDAO*





Rais João Lourenço (kushoto), amepata asilimia 51.2, dhidi ya asilimia 48.95 alizopata kiranja wa UNITA Costa Junior. **PICHA: MTANDAO**





# Bunge lahisi mwelekeo kushuka mapato halmashauri jiji Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa (LAAC), imebaini kuna mwelekeo wa kushuka kwa mapato ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutokana na chanzo kikubwa cha mauzo ya viwanja kutoendelea kufanya vizuri.

Akitoa maazimio ya LAAC, Makamu Mwenyekiti, Selemani Zedi, baada ya kuchambua hoja za ukaguzi za jiji hilo zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21, alisema vyanzo vipya vilivyobainishwa na Halmashauri hiyo mbele ya kamati hiyo ni Chinangali Park, maegesho ya malori Nala Soko la Ndugai, hoteli ya Dodoma City, kitegauchumi cha Mtumba na stendi ya kisasa.

Alisema wameona vyanzo hivyo ambavyo vitakuwa mbadala wa chanzo cha uuzaji viwanja ambacho sasa hakifanyi vizuri.

"Ni matumaini ya kamati sasa suala la kushuka mapato halitakuwapo tena kutokana na vyanzo mlivyovianisha na kile mnachotarajia kukusanya kupitia vyanzo hivyo, hivyo tunategemea mtakuwa na mwelekeo wa mapato unaokua," alisema.

Hata hivyo, alisema kamati haijaridhishwa na hatua ya kutopata mapato yoyote katika soko la Saba Saba.

"Taarifa ya CAG inaonesha kuwa Jiji la Dodoma lingeweza kupata takribani Sh. bilioni 1.2 kwa mwaka kutokana na tozo na ushuru katika soko hilo. Kamati hairidhishwi kuona Jiji la Dodoma halipati mapato katika soko la Sabasaba pamoja na kuwapo kwa biashara kubwa inayofanyika katika soko hilo,"alisema.

Zedi alisema kamati inakubaliana na mwelekeo wa mradi wa kujenga upya soko la kisasa kwa kushirikiana na wafanyabiashara waliopo kuanzia hatua ya usanifu na kutaka mabadiliko hayo yafanyike bila kuwapo migogoro.

"Kamati inatoa tahadhari kwa jiji kuhakikisha wanatumia eneo lao lenye hati kujenga soko jipya na endapo watataka kumshirikisha mmiliki wa eneo lililo jirani basi wahakikishe wanamakubaliano ya kimkataba ambayo hayana mgogoro,"alisema.

Zedi alisema kamati imetoa wiki mbili kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji hilo, Joseph Mafuru, kupeleka nyaraka zilizokamilika ofisi za CAG ili hoja ambazo zinapaswa kufungwa zifungwe ikiwamo ya kutoa zabuni bila bodi ya zabuni.

Kuhusu mishahara kwa wasiostahili, Makamu Mwenyekiti huyo alisema kamati imetoa miezi sita kwa jiji hilo kufuatilia na kuhakikisha Sh. milioni 51 zilizolipwa kwa watu hao zinarejeshwa.

Alisema fedha hizo zimelipwa kwa watumishi waliofariki dunia, waliostaafu, kusimamishwa kazi au kufukuzwa kazi.

"Hakikisheni mnafanya ufuatiliaji ndani ya miezi sita fedha zilizolipwa watu wasiostahili zirudishwe hazina ni fedha za serikali na hazipaswi kupotea,"alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati, Grace Tendega, aliitaka halmashauri hiyo kuhakikisha inafuata taratibu, kanuni na sheria na kuzingatia maelekezo ya CAG.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, aliihakikishia kamati kuwa maelekezo na maoni waliyotoa yatatekelezwa kwa Halmashauri zote za mkoa huo.



Mkurungenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemia Mchechu (kulia), akizungumza wakati alipokutana na wajumbe wa Kamati ya Bunge Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), jijini Dodoma jana. Kamati hiyo, ilipokea na kuchambua na kujadili taarifa ya Msajili wa hazina kuhusu uwekezaji katika shirika hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vifungashio vya plastiki vyazidi kutumika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKATI serikali ikiwa imetangaza kuanza rasmi kwa operesheni kabambe ya kutokomeza vifungashio vya plastiki ambavyo vimegeuka kuwa vibebeo kwenye mikoa yote nchini, bidhaa hiyo imeendelea kutumika kwa wingi katika maeneo mbalimbali likiwamo jiji la Dodoma.

Operesheni hiyo iliyotangazwa hivi karibuni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ilitarajiwa kuanza rasmi juzi kwenye mikoa yote nchini.

Jana, Nipashe ilifanya uchunguzi katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dodoma na kubaini wafanyabiashara wakiendelea kutumia mifuko hiyo kwa ajili ya kufangashia bidhaa zao.

Mmoja wa wafanyabiashara katika soko la Majengo, jijini hapa, Omary Hussein, alisema hawafahamu juu ya operesheni hiyo ya kupiga marufuku mifuko hiyo inayotumika sasa kama vifungashio.

"Hatujui kama mifuko hii inakatazwa sisi bado tunaendelea kutumia kama unavyoona kwa wafanyabiashara wengi hapa sokoni. Wote tunatumia mifuko hii kwa ajili ya kufungashia bidhaa mbalimbali na hatujaambiwa kitu chochote kuhusu operesheni hiyo na viongozi wetu," alisema Hussein.

Akizungumza na vyombo vya habari hivi karibu, Waziri Jafo alisema operesheni hiyo itagusa maeneo yote yakiwamo masoko, maduka, magulio, bucha za nyama na samaki. Pia alitoa miezi miwili kwa watendaji wake kupitia upya kanuni ili kubana vifungashio hivyo kugeuka kuwa vibebeo.

Dk. Jafo alitoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza na wataalamu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) waliokutana kujadili utekelezaji wa sheria ya mazingira.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliyeagiza mikoa yote nchini kuhakikisha wanapambana na matumizi ya mifuko ya plastiki.

"Operesheni hii itakuwa endelevu na usimamizi wa katazo la mifuko ya plastiki na masuala mengine ya kimazingira, kwahiyo itakuwa ni moja ya majukumu ya kawaida ya usimamizi wa mazingira kwa ngazi za Wilaya kupitia vyombo vya usalama ngazi za Wilaya pamoja na Maofisa Mazingira wa ndani ya Halmashauri kwa kushirikiana na NEMC," alisema. Alisema kanuni ya sita ya Mwaka 2019 ya kutokomeza mifuko ya plastiki ilipiga marufuku mifuko hiyo lakini iliruhusu vifungashio kwa lengo kubwa kwamba kuna baadhi ya bidhaa lakini kuna watu wasio waaminifu wamegeuza vifungashio kuwa vibebeo.

"Hivi karibuni tumekamata mizigo mbalimbali imekuwa ikitoka nje ya nchi na kukamatwa ikipita katika mipaka ya nchi, jambo hili haliridhishi hata kidogo,"alisema.

Aliwataka kwenye operesheni hiyo wakuu wa mikoa na wilaya wahakikishe wanashirikiana na viongozi wa masoko na magulio ili kuhakikisha mazingira yanakuwa salama.

## Serikali yaombwa kuwajali wahudumu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kuweka mikakati ya kuboresha maslahi ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii, wanaofanya kazi ya kuelimisha na kupinga masuala ya ukatili wa jinsia, ukeketaji na ndoa za ututoni vijijini ili kuimarisha sekta hiyo.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la People's Health Movement (PHM) Tanzania, Godfrey Philemon, wakati akifungua mkutano wa masuala ya afya uliohusisha asasi mbalimbali za kiraia.

Alisema ni vyema serikali ikaweka mikakati ya kuboresha maslahi ya wahudumu hao ambao muda mwingi wanazunguka katika maeneo ya vijijini kwa ajili ya kutoa elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia kwa jamii.

"Tunaiomba serikali iimarishe utaratibu wa wahudumu hao kwa sababu wanasaidia jamii katika utoaji elimu ya kupiga vita ukeketaji, "alisema Philemon.

Pilemon alisema pamoja na kuwa serikali inawatambua na sera ya afya inatambua mchango wao sasa ni wakati wa kuwa na mwongozo wa kitaifa kwenye kitengo hiko.

Alisema wakifanya hivyo itakuwa rahisi kuungana pamoja katika utoaji huduma jambo ambalo litasaidia kupunguza tatizo la watoa huduma hapa nchini.

Alisema baada ya mkutano huo moja ya mikakati waliyojiwekea ni kuhakikisha wanakutana na wahudumu hao ili kuwatambua pamoja na maeneo wanayofanyia kazi ili kujua kero zao.

Philemon alizitaja nchi zilizofanya vizuri katika kuwajali wahudumu ngazi ya afya ya jamii ni Burkina Faso, Ethiopia, Mali,Malawi,Tanzania na Uganda.

"Mfano nchi ya Malawi wana siku ya Kitaifa kwa ajili ya kutambua mchango wa wahudumu wa afya ya jamii na nchi nyingine zinawalipa na Tanzania tunahitaji kufikia hapo " alisema

Hata aliyeiomba serikali kuweka mikakati ya kuboresha maslahi ya wahudumu hao kwani wamekuwa wakifika maeneo ambayo watu wengine hawafiki kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya jamii.

Kwa upande wake Ofisa Uelimishaji na uhusiano kutoka PHM, Tanzania Thomas Edward alisema Shirika hilo limesajiliwa kama Asasi ya raia na linafanya kazi ya kuhakikisha huduma za afya kuwa haki kwa Watanzania wote.

"Kuangalia mijadala ya kisera, kuunga mkono jitihada za serikali katika kupaza sauti kwa watu wa kawaida," alisema.

Alisema kuwa kazi yao kubwa ni uelimishaji, utetezi ili kila mtu apate huduma ya afya katika kiwango kizuri

Alisema pia wanafanya kazi ya kuangalia sera zilizopo katika masuala ya uandaaji, kufanya tathimini ya miradi iliyopo kwenye masuala ya afya na suala la udhalilishaji wa kijinsia hususani kwa wanawake.



# Mil. 800/- kumaliza tatizo sugu maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SERIKALI imetoa zaidi ya Sh. milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji cha Mkunywa, Kata ya Madibira, Mbarali mkoani Mbeya na kwamba mradi huo baada ya kukamilika utahudumia vijiji saba.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Samuel Heche, alisema jana kuwa mradi huo ulianzishwa miaka 12 iliyopita lakini kutokana na sababu mbalimbali haukukamilika licha ya kutoa Sh. milioni 90 kwa wakati huo.

Alisema baada ya serikali kupata taarifa hizo, kupitia Wizara ya Maji ilitoa maagizo kwamba mradi huo ukamilike haraka na wananchi wa Madibira waanze kupata maji safi na salama.

"Kwa sasa mradi huo umefikia hatua mbalimbali na RUWASA wanaendelea kusimamia kazi usiku na mchana ili kumaliza na kutoa huduma kwa vijiji vingine vikiwemo Iheha, Mahango, Chalisuka, Mkunywa, Ikoga, Nyamakuyu na Nyakadete," alisema.

Mhandisi Heche alisema mkandarasi wa ujenzi katika mradi huo amekabidhiwa juzi na kwamba unatarajiwa kukamilika Februari, mwakani.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, alitembelea mradi huo na kushangazwa kwa nini haujakamilika kwa wakati licha ya serikali kutoa fedha.

Alisema mradi huo ni miongoni mwa miradi kichefuchefu katika Wizara ya Maji na kwamba hawatakubali kuona unakwama tena na badala yake RUWASA isimamie kuhakikisha wananchi wanaanza kupata huduma ya maji safi na salama.

Baada ya kukagua mradi huo, Mahundi alizungumza na wakazi wa madibira na kumueleza adha wanazopitia kutokana na tatizo la maji katika maeneo yao.

Secila Chungu alisema ndoa yake iko hatarini kuvunjika kutokana na muda mwingi kuutumia kutafuta maji na kushindwa kuhudumia ndoa yake.

Alisema zaidi ya masaa nane hutumia kwenda kutafuta maji hali inayosababisha mumewe kuona hapati nafasi ya kukaa kwa pamoja kupanga mipango.

Aliiomba serikali kukamilisha mradi huo ili waanze kupata huduma za maji safi na salama kwani miaka 12 imepita tangu kuanza ujenzi wa mradi huo lakini haukukamilika.

Alisema wanawake ndio wahanga wakubwa wa tatizo la maji kwani yanahitajika kwa ajili ya shughuli nyingi katika familia hivyo kukamilika kwa mradi huo kutasaidia ndoa zao kuwa salama na mambo mengine kufanyika.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Rueben Mfune amesema yeye ni jicho la Rais hivyo atahakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati na kujengwa katika viwango vinavyohitajika kwa kuzingatia thamani ya fedha.



Mkuu wa Polisi kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Yusuph Kamotta (kulia) na Mkuu wa Operesheni mkoani humo, Abdi Issango (kushoto), wakikagua stika ya viakisi mwanga ambavyo viliwekwa kwenye trekta kama mfano, wakati wakitoa elimu kwa madereva wilayani Mbarali juzi, kwa lengo la kuhamasisha uwekaji wa stika hizo, kabla ya kesho. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Watakiwa kuzingatia ukomo matumizi dawa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imewakumbusha wafanyabiashara na wauzaji wa dawa kuzingatia ukomo wa matumizi ya dawa na vifaa tiba wanavyoviuza ili kulinda afya za wananchi.

Rai hiyo imetolewa jana na Meneja wa TMDA Kanda ya Nyanda za juu Kusini, Anitha Mshighati, huku akisema wanatarajia kuanza ukaguzi katika kila duka la dawa kuangalia utekelezaji wa maagizo kuhusu marufuku ya kuuza dawa zilizokwisha muda wa matumizi.

"Wafanyabiashara wanapaswa kuzingatia kanuni na taratibu zilizotolewa na TMDA katika uuzaji wa dawa ili kukabiliana na uuzaji holela wa dawa ambazo zimekwisha muda au hazitakiwi mwa mujibu wa wataalam kwenye maduka ya dawa," alisema Mshighati.

Aliogeza kuwa licha ya kutangaza kufanya msako duka kwa duka kukagua utekelezaji wa agizo la marufuku uuzaji wa dawa zilizokwisha muda, aliwasisitiza wafanyabiashara kuwa na nakala ya kielektroniki ya taarifa ya mzigo mfano ankara, kifani pamoja na vibali kutoka taasisi zinazohusika na usajili.

Alisema wafanyabiashara hao wanatakiwa kuhakikisha wanajaza fomu ya usajili ya mteja na kuiwasilisha ofisi za TMDA ili kupata namba ya utambulisho na nywila.

Mshighati aliongeza kuwa kabla ya muhitaji kulipa ada ahakikishe anawasilisha hati ya malipo ambayo yatafanyika benki katika ofisi ya TMDA ili kupata kibali za kufanya biashara hiyo ya uingizwaji wa bidhaa anazozihitaji.

"Tunahamasisha wafanyabiashara wanaojihusisha na uuzaji wa dawa za binadamu kuzingatia utaratibu na sheria za kuingiza na kutoa bidhaa nchini ili kulinda afya za watumiaji," alisema Mshighati.

Aliwahamasisha wafanyabiashara kuzingatia usajili wa dawa nchini kujihakikishia kuwa zinakidhi viwango vya ubora, usalama na ufanisi ili watumiaji waweze kupata dawa sahihi kwa ugonjwa husika.

# Wasioweka viakisi mwanga vyombo vya usafiri kukiona

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Mbeya, limesema hadi kufikia Septemba Mosi, mwaka huu, wamiliki na madereva wa vyombo vya moto vikiwamo magari, pikipiki zote za magurudumu matatu na trekta wawe wameweka viakisi mwanga ili kukabiliana na ajali za barabarani. Maagizo hayo yalitolewa juzi na Mkuu wa Oparesheni Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Abdi Issango, wakati akimwakilisha Kamanda wa Polisi mkoani hapa , Ulrich Matei, kwenye ufunguzi wa mafunzo ya viakisi mwanga yaliyofanyika wilayani Mbarali.

Alisema Jeshi la Polisi limetoa elimu kuhusu umuhimu wa vyombo vya moto kuwekwa viakisi mwanga ili kukabiliana na ajali hususani nyakati za usiku na kwamba baada ya hapo oparesheni ya kuwakamata madereva wakaidi itaanza.

"Leo tumeanza kutoa elimu kwa madereva wa maguta, trekta, bajaji na Coaster lakini elimu hii ni kwa wote. Tunatekeleza maagizo ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camilius Wambura, kwamba kila mkoa utoe elimu ya umuhimu wa viakisi mwanga," alisema Issango.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Yusuph Kamotta, alisema miongoni mwa mikakati ya kupunguza ajali mkoani hapa ni pamoja na kuwekwa viakisi mwanga kwenye vyombo vya moto.

Alisema wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa maeneo yenye vyombo vingi vya usafiri ambapo kwa sasa kuna power tiller 3,000 ambazo zinatumika kusafirisha abiria na shughuli za kilimo.

"Tumetoa elimu kwa madereva na kuwaonyesha namna wanavyotakiwa kuweka viakisi mwanga kwenye vyombo vya moto. Naamini kila mmiliki au dereva atatekeleza agizo hili kwa mujibu wa sheria barabarani," alisema Kamota.

Aidha, Kamota alipiga marufuku madereva wa maguta na power tiller wilayani Mbarali kuacha tabia ya kusafirisha abiria kwani vyombo hivyo ni maalum kwa ajili ya kusafirisha mizigo.

Helson Zabron, mmiliki wa pawatila alisema elimu ya viakisi mwanga imekuja wakati muafaka na kwamba wako tayari kulitekeleza. Alisema atakuwa balozi mzuri kwa wenzake kuhamasisha kuweka viakisi mwanga kwenye vyombo vyao ili kuzuia ajali hususani nyakati za usiku.

Ofisa Mtendaji wa Ubaruku, Ponsiano Mhavila alilihakikishia Jeshi la Polisi kwamba zoezi hilo litatelezwa kwa ufanisi mkubwa na kwamba dereva yeyote atakayekaidi ataripotiwa kwenye vyombo vya sheria.



## Mkakati kudhibiti biashara binadamu kuimarishwa zaidi Waziri asema

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema serikali itaendelea kupambana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu kama inavyopambana na dawa za kulevya na udhalilishaji.

Aliyasema hayo jana katika hoteli ya Golden Tulip, visiwani hapa wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya siku ya kupinga usafirishaji haramu wa binadamu na uzinduzi wa mpango wa usimamizi wa nyumba salama.

Haroun, alisema kitendo cha Tanzania kuridhia mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia Biashara ya Binadamu ni dhahiri kuwa iko katika kupambana na janga hilo ambapo Zanzibar inatekeleza maadhimisho hayo.

Waziri huyo alisema biashara haramu ni vita katili na huchukua sehemu kubwa ya mapato haramu na waathirika wakuu ni wanawake na watoto.

Alisema, si vibaya wananchi kwenda kufanya kazi nje ya nchi lakini kutumikishwa kinyume cha sheria na taratibu haikubaliki.

Pia, alisema sababu za kuwapo kwa biashara haramu duniani kote ni uhitaji wa nguvu ikiwamo wananchi kutumikishwa katika viwanda, mashamba, migodi na maeneo mengine ambapo husababisha vitendo vya udhalilishaji.

Naye Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema kuzinduliwa kwa mwongozo huo ni mkakati wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu na ukatili kwa kuweka nyumba salama kwa ajili ya kuwasaidia waathirika.

Alisema kuna mafanikio mbalimbali yaliyopatikana ikiwamo kuwa na sheria ya usafirishaji haramu wa binaadamu lakini pia nguvu za ziada zinahitajika katika mapambano hayo.

# Hemed awapa kibarua walimu wakuu

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka walimu wakuu katika mkoa wa Kaskazini Pemba kuwajibika ipasavyo ili kuleta ufanisi wa kazi zao.

Hemed, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na walimu wakuu wa shule za maandalizi, msingi na sekondari za serikali na binafsi kwenye kikao kazi kilichofanyika kwenye ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Wete.

Alisema, walimu wakuu ndio wasimamizi wakubwa kwenye sekta ya elimu, hivyo aliwataka kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na kila mmoja kutimiza wajibu wake kwa maslahi ya taifa.

"Suala la nidhamu naomba walimu wakuu acheni muhali. Kuna walimu hawaji kazini kwa wakati, watoro, hawana mwongozo katika kufundisha. Hili lifuatilieni kwa nguvu zote ili kupata wataalamu na viongozi bora baadaye," alisema.

Hemed, alisema ni vyema kila mwalimu mkuu kuhakikisha anatoa mwongozo kwa walimu walioko chini yake ili kujua maslahi yao na kuwapatia haki zao na kuimarisha utawala bora.

Makamu huyo wa Rais , aliutaka uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha inawalipa walimu wote wanaodai stahiki zao ili kufanya kazi kwa weledi na kutoa wataalamu bora baadae.

Aidha, Hemed alisema kuwa Serikali itahakikisha inawalipa walimu wote stahiki zao ikiwemo fedha za likizo hata waliokuwa kwenye ugatuzi.

"Kila anayestahili kupata haki yake serikali itahakikisha analipwa kupitia utaratibu uliowekwa ili kufanya kazi kwa weledi mkubwa na kuhakikisha wanapatikana wataalamu na viongozi bora wa hapo baadae" alisema.

Pia, aliutaka uongozi wa wizara hiyo kuhakikisha ajira ambazo zimetangazwa na serikali zifate utaratibu ambao utasaidia kuwapata walimu ambao wanasifa stahiki.

Aidha, aliiagiza wizara kuhakikisha kila mwalimu atakaeajiriwa kufanya kazi katika sehemu husika ni vyema uongozi kusimamia mfanyakazi huyo akaende sehemu aliyooomba na si vinginevyo.

"Wizara ihakikishe nyumba ambazo zimejengwa kwa ajili ya walimu kupatiwa walimu husika na si kukaa mtu yeyote ambaye hahusiki kuishi humo," alisema.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohmed Mussa, alisema serikali imejipanga kuhakikisha inaimarisha na kuboresha shule zote ambazo zinataka kufanyiwa ukarabati kupitia pesa za ahuweni ya UVIKO -19.

Waziri Lela, alisema wizara itahakikisha inachukua hatua stahiki kwa walimu wote wa shule za serikali na binafsi ili kuhakikisha serikali inayafikia malengo ambayo imejiwekea kwa wananchi wake.



Waziri wa Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe (wa tano kulia mstari wa mbele), akiwa na wajumbe wa kamati ya ustawi wa jamii ya Baraza la Wawakilishi, baada ya kikao cha kujadili sheria ya mtoto, Chukwani, Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yajizatiti kuboresha mazingira uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar, imeanza kuchukua hatua za kuimarisha mazingira ya uwekezaji ili kukuza uchumi wa nchi na watu wake.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, aliyasema hayo jana mjini Zanzibar wakati akifungua kongamano la wafanyabiashara wa Iran na Zanzibar.

Aliyataja maboresho hayo ni pamoja na kufanya mabadiliko ya sheria, kisera na kuboresha huduma za kituo cha pamoja katika Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

Waziri aliitaja mikakati ya kuboresha miundombinu ya nchi ikiwamo ujenzi wa bandari ya Mangapwani, ujenzi wa barabara na kuongeza gridi ya umeme kwa kuongeza megawati 150.

Pia, aliwataka wafanyabiashara kutoka Jamhuri ya Kiislamu ya Iran kuwekeza visiwani hapa kutokana na fursa mbalimbali zilizopo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar SMZ iko tayari kushirikiana na wafanyabiashara hao katika masuala ya uwekezaji katika kupanua wigo kwenye sekta mbalimbali.

Waziri huyo alisema Zanzibar kuna fursa nyingi za kuwekeza ikiwamo uchumi wa bluu ambao umegusa sehemu nyingi za kuleta mafanikio.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo wa Iran, Seyed Mohammad Aghamiri, alisema nchi yake iko tayari kuwekeza visiwani hapa katika sekta mbalimbali .

Alisema uwekezaji huo utaleta maendeleo ya kielimu ili kwenda na kasi ya kiuchumi inayotakiwa. Pia, alisema Iran iko tayari kuwekeza katika masuala ya kilimo, ufugaji, uvuvi pamoja na utengezaji wa chanjo za mifugo.

Aidha, alisema Iran imetoa fursa kwa wadau kwenda nchini humo kupata mafunzo kuhusu utengenezaji wa chanjo hizo huku akiwataka washiriki wa kongamano hilo kulitumia katika kufungua na kukomaza mahusiano zaidi kibiashara.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji, Dk. Habiba Hassan Omar, alisema ujio wa wageni hao ni muhimu kwa kuwa utasaidia kuzitangaza fursa za nchi hizo mbili.

Alisema, kongamano hilo litaleta manufaa baina ya Iran na Zanzibar kuweza kushirikiana katika maeneo waliyoyaona.

"Kikao hichi kitakua na manufaa kwa pande zote mbili ambapo tutaweza kuzitumia fursa katika nchi zetu hizi mbili ili kuweza kufanya maamuzi ya uekezaji," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JACQUELINE ELLY MASONGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye namba za usajili **T446 DGG,** chasisi namba **ZCA250003650** , engine namba **1ZZ1065471,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

**DSM/RHQ/RB/338047/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NTIMI NIKUSUMA MTAWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0120-0101** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia K**IGONSERA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2002.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA : DAR/URA/RB/338476/2022**

**MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na mteja wetu **HERITAGE FINANCING CO. LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara mali ya Mapinduzi Aloyce Jeremiah (mdaiwa), itauzwa kufidia deni analodaiwa.

| JINA LA MDAIWA | MALI ITAYOUZWA | USAJILI | SIKU YA MNADA |
|---|---|---|---|
| MAPINDUZI ALOYCE JEREMIAH | PIKIPIKI | MC 684 CEX | 05/09/2022 |

**MASHARTI YA MNADA**

- Mnada utafanyika saa nne (4:00) asubuhi
- Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei yam nada papohapo na 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa mnada utarudiwa na pesa haitarudishwi.
- Gharama za kubadili umuliki ni juu ya mnunuzi
- Masharti ya mnada kuzingatiwa

**KWA MAWASILIANO PIGA 0735 170 553**

**KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD COURT BROKER**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA UHUMA FINANCIAL SERVICES TUTAFANYA MNADA WA HADHARA TAREHE 28/09/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA NYUMBA PLOT NO. 3 BLOCK 81 CHINANGALI EAST MALI YA HELI MWAFUTE. NA GARI T 425 AGR ESCUDO MALI YA ANDREW MNGUU BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MIKOPO YAO, MNADA WA GARI UTAFANYIKA NYERERE SQUARE WA NYUMBA UTAFANYIKA AREA' A' MAHALI NYUMBA ILIPO.

**KWA MAWASILIANO PIGA NO. 0688729841/ 0657222838**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.86 OF 2022**

**In the matter of the estate of the late EFRASIA KALIKAMO of DODOMA**

**AND**

**In the matter of an Application for letters of Administration by DOROTHY STEWART KALIKAMO**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 7 Day of 10,2022.

Dated at Dodoma this 6TH day of June, 2022.

PETITIONER

Presented for filling this 9 Day of 6 2022

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA AKDI YA GARI

**ALICIA LORI DAVIS** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX-D/CABIN** yenye namba za usajili **T826 ABX**, chasis namba In**1060057660**,engine namba **312690035**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa**

**ARU/ARU/RB/342717/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**

**SHAURI LA MADAI NA 196 YA MWAKA 2020**

**GATEWAY TO ZANZIBAR LTD..........MDAI**

**DHIDI YA**

**BENY BILLY CONSTRUCTION LTD......MDAIWA**

**KWA.BENY BILLY CONSTRUCTION LTD**

**KUITWA SHAURINI**

Kwakuwa mwombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo ya mwombaji yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii,mnahitajika kuhudhuria ninyi binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa kisheria,siku ya tarehe 6/9/2022 saa 07:00 mchana ili kusikiliza hukumu ambayo ilisikilzwa upande mmoja(mdai),mbele ya MHE.RUGEMALIRA.

**ANGALIZO**

Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu,mahakama ikitibitika kama mmepokea kuitwa shaurini,itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe....mwezi 08 mwaka 2022

HAKIMU MKAZI MKUU KISUTU -DAR ES SALAAM

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAMISA ISMAIL MAGOHA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3815-0013** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia VITIRA SECONDARY SCHOOL mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI CONTROL NAMBA: **9910834104754**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**

**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB. NA. MMC/LD/12497**

**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: AMRI RAMADHANI NG'UMBEWE WA S.L.P 222, MOROGORO**

**ARDHI: KIWANJA NA. 91 KITALU BB MOROGORO TOWNSHIP-MANISPAA YA MOROGORO**

**MUOMBAJI: RAMADHANI AMRI RAMADHANI WA S.L.P 3017, MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa SIKU 30 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti. **HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa MKURUGENZI WA MANISPAA-MOROGORO S.L.P166 MOROGORO

Valency H.K

KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANNETH DOTTO NUSURUPIA**

ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T114 DMC**

ENGINE NAMBA **2AZEAA901989**

CHASSES NAMBA

**ACA385144260**

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU

TAARIFA:- **ARU/ARU/RB 198854/2022**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ARNOLD LEORNALD SAKAYA** anatangaza kupotea kwa RESULT SLIP ya kidato cha sita yenye index namba **S.12220/0504** iliyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MSAMALA SECONDARY SCHOOL mwaka 2022 . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **MKB/RB/2726/2022**

***OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni IndustRial***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## 18 wapigwa risasi na polisi Madagascar

WATU 18 wakazi wa mji wa Ikolo nchini Madagascar wamefariki huku wengine wakijeruhiwa baada ya polisi kufyatua risasi ili kutawanya kundi la watu waliokuwa wamekasirishwa kwa kutekwa nyara kwa mtoto mwenye ulemavu wa ngozi/albino.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AFP, ripoti hiyo imetolewa na Tango Oscar Toky ambaye ni daktari mkuu kwenye hospitali moja kusini mashariki mwa Madagascar.

Toky alisema kati ya watu 34 waliojeruhiwa, tisa ni mahututi, na kwamba wanasubiri helikopta za serikali ili kuwapeleka kwenye hospitali ya mji mkuu.

"Takriban watu 500 waliokuwa wamebeba visu na mapanga walijaribu kuingia kwa nguvu kwenye kituo cha polisi ambako washukiwa wa utekaji nyara walikuwa wameshikiliwa," alisema.

Ofisa wa polisi kutoka mji wa Ikongo, akizungumza kwa njia ya simu na AFP alisema walijaribu kushauriana na waandamanaji hao lakini pale walipokataa kusikia, hawakuwa na njia nyingine ila kutumia risasi za moto ili kujilinda.

Mkuu wa polisi kitaifa Andry Rakotondrazaka aliwaambia wanahabari kwamba tukio hilo ni la kuhuzunisha, na kwamba lingezuilika.

**VOA**

**"Takriban watu 500 waliokuwa wamebeba visu na mapanga walijaribu kuingia kwa nguvu kwenye kituo cha polisi ambako washukiwa wa utekaji nyara walikuwa wameshikiliwa," alisema.**

# 20 wauawa machafuko Iraq, Iran yafunga mpaka

**BAGHDAD, IRAQ**

MACHAFUKO mapya yametajwa kuikumba Iraq na kusababisha vifo vya watu takribani 20 huku Iran ikifunga mipaka yake wakati wanamgambo wa ulamaa wa Kishia wenye ushawishi mkubwa wakikabiliana na vyombo vya usalama katika eneo la Green Zone.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, wanamgambo wa Saraya Salam wanaotajwa kuegemea upande wa Muqtadha al-Sadr walirusha mabomu kwa kutumia makombora kuelekea eneo la Al-Mintagah wakati vyombo vya usalama vya Iraq vikijibu kwa mashambulizi.

Jeshi la Iraq lilisema makombora manne yalirushwa kuelekea eneo hilo ambalo lina ulinzi mkali.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa picha za moja kwa moja za televisheni zilionesha ghasia hizo, huku mtu mmoja akijeruhiwa karibu na jengo la wizara ya mambo ya kigeni ya Iraq. Ilielezwa kuwa idadi ya waliouawa tangu machafuko yalipoanza Agosti 29 ilikuwa imefikia 22 kwa mujibu wa maofisa wawili wa afya walionukuliwa na shirika la habari la Associated Press.

Taarifa ilisema wanamgambo wa Saraya Salam waliamua kukabiliana na vikosi vya usalama vya Iraq kulipiza kisasi mauaji ya wafuasi wa al-Sadr wasiokuwa na silaha.

Kwa mujibu wa maofisa wawili wa vyombo vya usalama waliozungumza na shirika la habari la Reuters, wanamgambo hao pia walitwaa udhibiti wa makao makuu ya kundi jengine la wanamgambo wanaoungwa mkono na Iran katika miji ya kusini mwa Iraq usiku wa kuamkia jana.

**IRAN YAFUNGA MPAKA**

Iran, ambayo inashutumiwa na upande wa Al-Sadr kwa kujihusisha na siasa za ndani za Iraq, ilitangaza kufunga mpaka wake kwa kile ilichosema ni kwa sababu ya machafuko na amri ya kutotoka nje iliyotangazwa katika baadhi ya maeneo nchini Iraq.

Televisheni ya serikali ya Iran iliwataka raia wa nchi hiyo kuepuka safari za kwenda Iraq na kwa mahujaji wake waliokuwa tayari ndani ya Iraq kutokwenda kwenye miji mingine kando na waliyopo sasa.

Mamilioni ya Wairani huzuru mji wa Kerbala nchini Iraq kila mwaka kushiriki maadhimisho ya siku 40 za kuomboleza mauaji ya Hussein, mmoja wa wajukuu wa Mtume Muhammad (S.A.W).

**MKWAMO WA KISIASA**

Serikali ya Iraq ipo kwenye mkwamo wa kisiasa tangu chama cha Al-Sadr kushinda wingi wa viti kwenye uchaguzi wa bunge wa mwezi Oktoba, lakini kushindwa kupata viti vya kutosha kuunda serikali peke yake.

Ilielezwa kuwa hadi kuamuwa kujiondowa kwenye majukumu yote ya kisiasa wiki hii, ulamaa huyo alikuwa amekataa kutafuta muafaka na mahasimu wake wanaoungwa mkono na Iran na alijitoa kwenye mazungumzo ya kuutatua mkwamo huo. Pia taarifa hiyo ilisema hatua ya hivi karibuni ya kujiuzuru ghafla imeugeuza mkwamo huo wa kisiasa kuwa machafuko, huku pakiwa hapajulikani hatima yake.

Vile vile ilidaiwa kuwa ulamaa huyo anajipatia nguvu kubwa kutokana na uwezo wake wa kuhamasisha umma na kudhibiti sehemu kubwa ya wafuasi wake walio kwenye ngazi za mashina, lakini tamko lake la kuachana na siasa liliashiria kuwapa wafuasi wake uhuru wa kujiamulia na kujitendea watakavyo.

***DW***



Vikosi vya usalama vikitumia gesi ya kutoa machozi kuwatawanya waandamanaji kutoka Ikulu ya Jamhuri mjini Baghdad juzi. **PICHA: DW.**

# Visa watu kutoweka vyakithiri Mexico

**MEXICO, MEXICO**

UMOJA wa Mataifa (UN) imesema mkakati wa kikatili wa kutisha raia ni tatizo la kimataifa lakini nchini Mexico ambako watu 100,000 wametoweka tangu 1964 inatajwa kuwa inaleta sura mbaya kwa nchi tangu mwaka 2014.

Agosti 30 ni siku ya kimataifa ya kukumbuka manusura na waathirika wa vitendo vya kutoweshwa duniani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI, suala la kutoweka kwa wanafunzi 43 bado halijapatiwa ufumbuzi.

Mwaka 2021 kamati dhidi ya vitendo vya kutoweshwa ambayo iko ziarani nchini Mexico ilisema ina wasiwasi juu ya hali inayoojiri nchini humo na hali ya unyanyasaji inayoathiri waathiriwa na familia zao katika muktadha ambapo wahusika hawaadhibiwi.

Ilielezwa kuwa miongoni mwa watu waliotoweka ni wanafunzi 43 wa Ayotzinapa, waliotekwa nyara usiku wa Septemba 26 kuamkia Septemba 27, 2014 huku jambo hilo likitajwa kuzua sintofahamu nchini Mexico na ufichuzi mpya wa hivi majuzi ambao unaonyesha kuwa kesi hiyo ni uhalifu wa serikali ambayo inaendelea kutikisa Mexico juu ya tatizo hilo.

Aidha, ilibainishwa kuwa miaka nane baadaye mabaki ya miili ya wanafunzi watatu pekee kati ya 43 ndiyo yaliyopatikana.

Akija kusaidia familia wakati wa maandamano ya kutafuta haki, Juventina Nicolas, kutoka shirika linalopambana dhidi ya mateso na kutokujali, alisisitiza utafiti na uchunguzi havipaswi kusitishwa.

"Hii ni miaka nane ya maandamano, utafiti na mateso kwa wazazi kwa huzuni kubwa kwa sababu bado hakuna haki, tunachotaka ni kujua wapi walipo hawa waliotoweka," alisema Nicolas.

Mmoja wa wajumbe wa shirika linalotetea haki kwa wahanga waliotoweka Angelica Orozco, alieleza kuwa "Vita hivi ambavyo Felipe Calderon alivianzisha mwaka wa 2006 na ambavyo vilileta wimbi hili zima la umwagaji damu na kutoweka kwa watu kote Mexico vilituathiri sote moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja," alisema.

Aliongeza kuwa shirika lao linaambatana na familia kukabiliana, kutojali na kutochukua hatua kwa mamlaka, akidai kuwa mara nyingi ni ndugu wenyewe ambao huchunguza na kutafuta kupotea kwao.

"Lengo letu siku zote litakuwa kuwatafuta, tunaweza kuona kwamba si polisi wala tume ya utafiti ya ndani yenye nia yoyote ya kubadilisha mambo," alibainisha.

Inaelezwa kuwa nchini Mexico, katika idadi kubwa ya visa vya watu kutoweshwa, hakuna mhalifu anayeadhibiwa.

***RFI***

# KMKM, KIPANGA KAMILI KUWANIA NGAO YA JAMII

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wanatarajia kuwakaribisha vinara wa Kombe la FA, Kipanga FC katika mechi ya kuwania Ngao ya Jamii itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Mchezo huo utakaoanza saa 11:00 jioni ni maalumu kwa ajili ya kufungua pazia la Ligi Kuu Zanzibar msimu mpya wa 2022/2023.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Bakari, alisema maandalizi ya mchezo huo yako katika hatua za mwisho na wanatarajia timu zote zitaonyesha soka la kuvutia.

Bakari alisema kamati yake inaendelea na jitihada za kukamilisha mambo yote muhimu yanakamilika kwa asilimia 100 kabla ya muda wa mchezo huo haujafika.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema matarajio yake ni kuona kikosi chake kinapambana na kuhakikisha wanabeba ngao hiyo msimu huu.

Msimu alisema timu yake imefanya maandalizi mazuri na anaamini wachezaji wake watatekeleza yale waliyojipanga na hatimaye kuanza msimu mpya kwa kutwaa ubingwa huo.

"Tunawaheshimu wapinzani wetu, tunajua mchezo utakuwa mgumu sana kwa sababu sote tumejiandaa kuchukua ngao hiyo, kufanya vizuri katika Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa, japo sisi tunahitaji kunyakuwa ngao hii tuliyoikosa msimu uliopita," Bakari alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Kipanga, Khamis Hassan, alisema wachezaji wake wote wana morali na wamejipanga kucheza vyema ili kuibuka na ushindi katika mechi ya leo.

Hassan alisema timu yake imejiandaa kutimiza malengo manne ikiwamo kubeba Ngao ya Jamii, kutetea ubingwa wa Kombe la FA na kufanya vyema katika Ligi Kuu Zanzibar.

"Lakini pia tuna malengo ya kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, hatutaki kutolewa mapema, tutapambana na tumedhamiria kufika mbali," aliongeza Hassan.

Kocha huyo pia amewataka mashabiki wa soka Zanzibar kujitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Amaan kuwashangilia na kwa kufanya hivyo, itawapa hamasa wachezaji wa timu hizo.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Gongo la Mboto wakifanya mazoezi ya mpira wa magongo kwa ajili ya kujiandaa na mashindano mbalimbali watakayoshiriki kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete Youth Park jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# KMC yaitangazia vita Simba

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kuanza msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kusuasua, Kocha Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, amesema anautumia vyema muda wa mapumziko kukiimarisha kikosi chake na hatimaye kurejea dimbani kikiwa na nguvu mpya.

KMC ilianza msimu mpya kwa kufungwa na Coastal Union bao 1-0 na mchezo wake wa pili ililazimishwa sare ya magoli 2-2 dhidi ya Polisi Tanzania.

Hitimana aliliambia gazeti hili baada ya kutofanya vyema katika michezo miwili ya awali, alibaini safu yake ya ulinzi ilikuwa na mapingufu ambayo sasa ameyafanyia kazi kwa ajili ya kupata ushindi katika mechi inayofuata.

"Msimu uliopita tulikuwa na tatizo na beki ya kati, tumefanya usajili katika eneo hilo, naendelea kutengeneza muunganiko mzuri wa kikosi kwa kuboresha kuanzia eneo la ulinzi, viungo na ushambuliaji,".

"Tunatumia mapumziko haya kucheza mechi za kirafiki ili kujiweka vizuri na tutakaporejea katika ligi, tunahitaji kuja kivingine zaidi kwa kupata ushindi katika michezo iliyopo mbele yetu ikiwamo dhidi ya Simba," alisema Hitimana.

Aliongeza wamejiandaa kucheza kwa tahadhari katika mechi yao inayofuata dhidi ya Simba huku akisifia kikosi alichokisajili kitasaidia kumpa matokeo chanya.

## Wasanii chipukizi kusakwa Novemba

**Na Saada Akida**

KAMPUNI ya Music Africa of Canada Inc imeandaa tamasha la kuibua vipaji vya wasanii mbalimbali chipukizi ambalo litajulikana kwa jina Afrofest litakalofanyika Novemba, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Tamasha hilo la Afrofest litajumuisha muziki na tamaduni za kiafrika ambalo kwa mara ya kwanza lilifanyika mwaka 1989 nchini Canada na Afrika limefanyika mara moja huko Ghana mwaka 2019.

Kwa hapa nchini, tamasha hilo linafanyika kwa mara ya pili.

Akizungumza jijini jana, Rais wa Kampuni ya Music Africa of Canada Inc, Peter Toh, alisema wanatarajia kuanza mashindano mwezi ujao kwa kuwachuja na kupata wasanii 10 chipukizi ambao bado hawajaingia katika soko la kimataifa.

"Kutakuwa na wasanii watakaoalikwa katika tamasha kubwa la Afrofest litakalofanyika Toronto, Canada Julai mwakani," alisema Toh.

Aliongeza kampuni hiyo pia imejipanga kutoa elimu na ushauri kwa wasanii wa fani zote ambao watahitaji ili kuhakikisha wanafikia malengo yao huku akiweka wazi utaratibu wa kujiandikisha utawekwa wazi hivi karibuni.

## Prisons yaachana na 'pira' gwaride

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Prisons, Patrick Odhiambo, amebadilisha utaratibu na falasafa ya timu hiyo kutoka kucheza mfumo wa kukimbiza na kasi na sasa kuhamia kwenye soka la pasi nyingi.

Akizungumza na gazeti hili, Odhiambo alisema amelazimika kubadilisha aina ya uchezaji, kutokana na mwenendo na ushindi uliopo katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Odhiambo alisema anataka kuona wachezaji wake wanabadilika na kucheza soka la kuvutia ambapo anaamini litasaidia kuwapa matokeo chanya katika mechi mbalimbali watakazocheza.

"Mpira unabadilika, ni muhimu na sisi tukabadilika, siku hizi mpira uka kasi na pasi, watu wanafungua vyumba, na ndio falsafa yangu, nataka kuona wachezaji wetu wanaweza kumiliki mpira mguuni, wacheze soka la kisasa, kwa sasa mpira ni biashara, wanapaswa kujitangaza na kuitangaza klabu," alisema Odhiambo.

Kocha huyo aliongeza aliona mabadiliko ya kikosi chake katika mechi iliyopita dhidi ya Dodoma Jiji ambayo walipata ushindi wa mabao 2-1.

## ZISIKUPITE

### RONALDO ANUKIA NAPOLI
MSHAMBULIAJI, Cristiano Ronaldo anaweza kuondoka Manchester United na kuelekea Napoli wiki hii. Mshambuliaji wa United na Ureno mwenye umri wa miaka 37 ameanza mechi moja pekee ya Ligi Kuu England msimu huu. ***(Metro)***

### JAMES ATAJWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur ipo katika mazungumzo kuhusu uwezekano wa kumnunua winga wa Leeds United na Wales, Daniel James mwenye umri wa miaka 24, kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho. ***(Fabrizio Romano)***

### SPURS YAMFUATA CARRASCO
KLABU ya Tottenham Hotspur imefufua nia yao ya kumnunua kiungo wa kati wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Yannick Carrasco mwenye umri wa miaka 28. ***(Telegraph)***

### AUBAMEYANG SOKONI
CHELSEA inataka kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 33. ***(Guardian)***

### POTTER KUMRITHI GERRARD
KLABU ya Aston Villa imeonyesha nia ya kumchukua Kocha wa Brighton, Graham Potter kama mbadala wa Steven Gerrard, ambaye amepoteza mechi tatu kati ya nne za kwanza za Ligi Kuu England msimu huu. ***(Football Insider)***

### BAKAYOKO AGEUKA LULU
KLABU ya Newcastle United inamtaka kiungo wa kati wa Chelsea, Tiemoue Bakayoko mwenye umri wa miaka 28 ambaye yuko AC Milan kwa mkopo wa miaka miwili. Nottingham Forest pia wanamwania mchezaji huyo. ***(Calciomercato)***

### GALLAGHER ANUKIA PALACE
KLABU ya Crystal Palace imetoa ofa ya pauni milioni 27 kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 22. ***(Times)***

### BELLERIN KUTUA BETIS
BEKI wa Arsenal na Hispania, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 27, anaweza kujiunga na Real Betis, ambapo alikuwa kwa mkopo msimu uliopita. Bellerin hajaichezea Arsenal tangu Mei, mwaka jana. ***(Estadio Deportivo)***

### DE JONG KUBAKI BARCA
KIUNGO wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, atasalia katika klabu hiyo licha ya kuhusishwa na Manchester United na Chelsea wakati wa uhamisho wa majira ya joto. ***(Football Espana)***

### VILLA, WOLVES VITANI
ASTON Villa na Wolves zote zina nia ya kumsajili beki wa West Ham, Craig Dawson mwenye umri wa miaka 32. ***(Sun)***

### LUIZ ATAKIWA JUVENTUS
JUVENTUS itajaribu kumsajili kiungo wa kati wa Aston Villa na Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 24, wakishindwa kufikia makubaliano na Paris St-Germain kumhusu Leandro Paredes mwenye miaka 28 raa wa Argentina. ***(Sky Sport Italia).***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CONTE: NATAKA KANE ASAINI MKATABA MPYA

**Afunguka mshambuliaji huyo ana furaha zaidi akiwa klabuni hapo huku...**

**LONDON, England**

ANTONIO Conte amekiri anataka mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane asaini mkataba mpya na klabu hiyo.

Baada ya hali ya kutatanisha mwaka 2021 ambapo alishinikiza kuhamia Manchester City, nahodha huyo wa England alirejea katika kiwango bora na kuifungia Spurs mabao, na kuisaidia kukaa katika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu kwa magoli mawili dhidi ya Nottingham Forest, Jumapili.

90min ilifichua Julai kwamba, si Kane wala klabu waliokuwa katika mbio za kusaini mkataba mpya, huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwaka 2024.

Ana furaha zaidi chini ya Conte kuliko mtangulizi wake, Nuno Espirito Santo na Mtaliano huyo anaamini klabu hiyo inajaribu kumfanya akubali kumwaga wino katika mkataba mpya.

Alisema: "Lazima niwe mkweli, sijui kuhusu hali hii, sijui maelezo yaliyopo kwa sasa,"alisema Conte akinukuliwa na Daily Mail.

"Unajua tunazungumza juu ya mchezaji muhimu kwa Tottenham. Na nia ya kila mmoja ndani ya klabu ni (kwa Kane) kuendelea kusalia Tottenham, ili kusaini mkataba mpya.

"Lakini ukiniuliza kuhusu maelezo, kuhusu habari, siwezi kukujibu."

Ni Erling Haaland pekee (mabao sita) ambaye amefunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu kuliko Kane katika hatua hii ya mwanzo ya msimu.

Timu hiyo ya London Kaskazini imepitwa pointi mbili dhidi ya vinara wa mapema na wapinzani wa wa jiji moja Arsenal, pamoja na Manchester City na Brighton ambao pia wameandikisha pointi 10 katika michezo yao minne ya ufunguzi.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,027,3

JACKPOT
MECHI WIKI HII

TAREHE: 31 AGOSTI NA 02 SEPTEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 31/08/22 | 19:30 | Empoli vs Verona | 2.61 | 3.26 | 2.56 |
| 02. 31/08/22 | 19:30 | Udinese vs Fiorentina | 2.86 | 3.36 | 2.31 |
| 03. 31/08/22 | 20:00 | Angers vs Reims | 2.42 | 3.21 | 2.86 |
| 04. 31/08/22 | 21:00 | Rostov vs Dinamo Moscow | 2.60 | 3.18 | 2.50 |
| 05. 31/08/22 | 22:00 | Farul Constanta vs Steaua Bucuresti | 2.84 | 3.09 | 2.47 |
| 06. 02/09/22 | 03:30 | Atletico GO vs Sao Paulo | 2.84 | 3.04 | 2.39 |
| 07. 02/09/22 | 13:30 | Incheon Utd vs Gangwon | 2.65 | 3.24 | 2.42 |
| 08. 02/09/22 | 13:30 | Consadole Sapporo vs Cerezo Osaka | 2.54 | 3.27 | 2.49 |
| 09. 02/09/22 | 19:30 | Heidenheim vs Fortuna Dusseldorf | 2.43 | 3.26 | 2.76 |
| 10. 02/09/22 | 21:00 | Mezokovesdi SE vs Zalaegerszegi TE | 2.47 | 3.36 | 2.52 |
| 11. 02/09/22 | 21:45 | Le Havre vs Caen | 2.53 | 3.08 | 2.78 |
| 12. 02/09/22 | 22:00 | West Bromwich vs Burnley | 2.41 | 3.11 | 2.91 |
| 13. 02/09/22 | 22:00 | Leganes vs Eibar | 2.59 | 2.84 | 2.93 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WILLIAN AKARIBIA KURUDI EPL



**LONDON, England**

KIUNGO wa zamani wa Brazil, Willian anakaribia kurejea kwenye Ligi Kuu England (EPL), kwa kujiunga na Fulham.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea na Arsenal alikuwa akiichezea Corinthians ya Brazil.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alisitisha mkataba wake na klabu hiyo ya Brazil baada ya kudai yeye na familia yake walipokea vitisho vya kuuawa katika mitandao ya kijamii.

Kwa sasa anatarajia kufanyiwa vipimo vya afya yake kabla ya kujiunga na Fulham na ikibidi, dili hilo linaweza kukamilika baada ya dirisha la uhamisho kufungwa kutokana na hadhi ya mkataba wa Willian.

Willian, alishinda mataji matano, yakiwamo mawili ya Ligi Kuu England katika kipindi chake cha miaka saba akiwa Chelsea kabla ya kujiunga na Arsenal kwa mkataba wa miaka mitatu mwaka 2020.

Mkataba wake na Arsenal ulikatizwa baada ya mwaka mmoja kwa sababu hakufanya lolote na alihamia klabu yake ya kwanza ya Corinthians katika nchi yake.

Willian alikuwa mchezaji muhimu kwa Brazil baada ya kucheza kwa mara ya kwanza mwaka 2011, lakini aliichezea nchi yake mara ya mwisho mnamo 2019.

# Cavani atua rasmi Valencia

**VALENCIA, Hispania**

KLABU ya Valencia imethibitisha kumnasa mchezaji wa kimataifa wa Uruguay, Edinson Cavani huku mshambuliaji huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain na Manchester United akijiunga kwa mkataba wa miaka miwili.


Cavani, alikuwa mchezaji huru baada ya mkataba wake kumalizika kule Old Trafford mapema mwaka huu, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 tangu wakati huo alikuwa akiwindwa na klabu nyingi za Ulaya.

Lakini ni timu ya LaLiga ambayo mshambuliaji huyo mkongwe amechagua kujiunga nayo, akiungana na Kocha, Gennaro Gattuso kwa uhamisho wa bure, na mkataba wake unatarajiwa kumalizika Juni 2024.

Ni uhamisho unaomaanisha Cavani atakuwa amecheza Ligi Kuu nne kati ya tano za Ulaya.

Aliondoka Danubio katika nchi yake na kujiunga na Palermo kule Serie A, kabla ya kucheza na Napoli, Paris Saint-Germain na Manchester United.

Mshindi huyo mara sita wa Ligue 1 kule Parc des Princes, aliondoka kama mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo, akiwa na mabao 200 kwa jina lake, alipohamia Ligi Kuu England mwaka 2020.



## HABARI MICHEZO

393,141/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/09/22 | 17:00 | Swansea City vs Queens Park Rangers | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 02. 03/09/22 | 17:00 | Rotherham United vs Watford FC | 2.90 | 3.15 | 2.41 |
| 03. 03/09/22 | 19:00 | AC Milan vs Inter Milano | 2.60 | 3.25 | 2.60 |
| 04. 03/09/22 | 19:00 | FC Sion vs FC Basel 1893 | 2.60 | 3.30 | 2.50 |
| 05. 03/09/22 | 19:30 | Real Sociedad San Sebastian vs Atletico Madrid | 2.80 | 3.10 | 2.50 |
| 06. 03/09/22 | 19:30 | SD Ponferradina vs Sporting Gijon | 2.55 | 3.20 | 2.65 |
| 07. 03/09/22 | 20:00 | AC Omonia Nicosia vs AEK Larnaca | 2.50 | 3.35 | 2.60 |
| 08. 03/09/22 | 21:45 | Lazio Rome vs SSC Napoli | 2.80 | 3.35 | 2.36 |
| 09. 04/09/22 | 02:00 | New York Red Bulls vs Philadelphia Union | 2.35 | 3.45 | 2.75 |
| 10. 04/09/22 | 14:00 | Reading FC vs Stoke City | 2.85 | 3.15 | 2.43 |
| 11. 04/09/22 | 14:30 | Hansa Rostock vs Hannover 96 | 2.49 | 3.35 | 2.65 |
| 12. 04/09/22 | 15:00 | Odense Boldklub vs Viborg FF | 2.55 | 3.50 | 2.48 |
| 13. 04/09/22 | 16:00 | AC Ajaccio vs FC Lorient | 2.37 | 3.25 | 2.85 |
| 14. 04/09/22 | 16:00 | Stade Brest 29 vs Strasbourg Alsace | 2.90 | 3.40 | 2.28 |
| 15. 04/09/22 | 17:00 | Huddersfield Town vs Blackpool | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 16. 04/09/22 | 18:30 | Manchester United vs Arsenal FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 17. 04/09/22 | 21:30 | Aris Thessaloniki vs PAOK Thessaloniki | 2.39 | 3.15 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 31 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1394 | Avispa Fukuoka vs Gamba Osaka | 2.03 | 3.09 | 3.53 |
| 14:00 | 2720 | Chonburi vs Bangkok Glass | 3.63 | 3.29 | 1.92 |
| 16:00 | 1404 | Kairat Almaty vs Akzhaiyk Uralsk | 1.73 | 3.33 | 4.50 |
| 16:00 | 4602 | Taraz vs Shakhter Karagandy | 2.29 | 3.04 | 2.99 |
| 17:10 | 4076 | Al Ahli Doha SC vs Al Gharafa SC | 3.82 | 3.77 | 1.74 |
| 17:30 | 2111 | Javor Ivanjica vs Kolubara | 1.98 | 3.38 | 3.34 |
| 17:30 | 3184 | FK Vozdovac vs Radnik Surduluca | 1.60 | 3.68 | 4.91 |
| 17:30 | 3987 | Paide Linnameeskond vs Levadia Tallinn | 2.70 | 3.58 | 2.22 |
| 18:00 | 2714 | Paksi FC vs Kisvarda FC | 2.36 | 3.44 | 2.60 |
| 19:00 | 3671 | Spartak Trnava vs Liptovsky Mikulas | 1.35 | 4.60 | 7.04 |
| 19:00 | 4749 | Rakow Czestochowa vs Pogon Szczecin | 1.99 | 3.29 | 3.39 |
| 19:00 | 5409 | Zemplin Michalovce vs Ruzomberok | 2.65 | 3.23 | 2.42 |
| 19:15 | 5167 | KKS 1925 Kalisz vs Widzew Lodz | 5.91 | 4.43 | 1.42 |
| 19:20 | 2130 | Al Arabi Doha SC vs Lekhwiya SC | 2.60 | 3.68 | 2.25 |
| 19:30 | 2148 | Backa Topola vs FK Radnicki 1923 | 1.51 | 3.79 | 5.70 |
| 19:30 | 3541 | Sampdoria vs Lazio | 3.94 | 3.54 | 1.84 |
| 19:30 | 4255 | Empoli vs Verona | 2.59 | 3.24 | 2.59 |
| 19:30 | 4848 | Udinese vs Fiorentina | 2.64 | 3.34 | 2.48 |
| 19:45 | 1449 | PSV Eindhoven vs FC Volendam | 1.08 | 9.44 | 19.09 |
| 19:45 | 2379 | Hapoel Beer Sheva vs FC Ashdod | 1.50 | 4.11 | 5.29 |
| 20:00 | 2376 | Monaco vs Troyes | 1.36 | 5.02 | 7.23 |
| 20:00 | 2992 | Kristiansund vs Viking | 3.26 | 3.46 | 2.09 |
| 20:00 | 3759 | Tromso vs Stromsgodset | 1.97 | 3.47 | 3.57 |
| 20:00 | 3763 | Montpellier vs AC Ajaccio | 2.04 | 3.37 | 3.47 |
| 20:00 | 4007 | Lyon vs AJ Auxerre | 1.26 | 6.03 | 8.84 |
| 20:00 | 4026 | Strasbourg vs Nantes | 1.88 | 3.52 | 3.87 |
| 20:00 | 4982 | Angers vs Reims | 2.45 | 3.21 | 2.81 |
| 20:30 | 4885 | Videoton FC vs Kecskemeti TE | 1.48 | 3.92 | 5.88 |
| 21:00 | 3467 | Slavia Prague vs Teplice | 1.13 | 8.16 | 18.37 |
| 21:00 | 3949 | Partizan vs Red Star Belgrade | 2.76 | 3.15 | 2.38 |
| 21:30 | 1764 | Arsenal vs Aston Villa | 1.49 | 4.16 | 5.86 |
| 21:30 | 2904 | Vasas SC vs Ferencvaros TC | 5.29 | 4.02 | 1.51 |
| 21:30 | 3406 | Manchester City vs Nottingham | 1.10 | 8.33 | 19.16 |
| 21:30 | 4540 | Royal Antwerp vs Union Saint Gilloise | 2.66 | 3.32 | 2.51 |
| 21:30 | 5893 | Bournemouth vs Wolverhampton | 3.40 | 3.25 | 2.09 |
| 21:45 | 2137 | Napoli vs Lecce | 1.25 | 5.81 | 9.21 |
| 21:45 | 2232 | West Ham vs Tottenham | 3.51 | 3.61 | 1.93 |
| 21:45 | 3568 | Juventus vs Spezia | 1.30 | 4.97 | 9.20 |
| 21:45 | 4151 | Livingston vs Dundee Utd | 1.91 | 3.28 | 3.68 |
| 21:45 | 4776 | Sunderland vs Rotherham | 2.07 | 3.30 | 3.40 |
| 21:45 | 5013 | Ross County vs Celtic | 12.80 | 6.50 | 1.15 |
| 21:46 | 3365 | Viktoria Koln vs Bayern Munchen | 60.93 | 15.23 | 1.02 |
| 22:00 | 2126 | Rennes vs Brest | 1.45 | 4.51 | 6.02 |
| 22:00 | 2509 | Marseille vs Clermont Foot | 1.36 | 4.82 | 7.43 |
| 22:00 | 2932 | Lille vs Nice | 1.99 | 3.42 | 3.57 |
| 22:00 | 3101 | Toulouse vs Paris St Germain | 9.92 | 5.95 | 1.24 |
| 22:00 | 3454 | Blackpool vs Blackburn | 2.31 | 3.19 | 2.99 |
| 22:00 | 3460 | Lens vs Lorient | 1.53 | 4.12 | 5.63 |
| 22:00 | 4198 | Liverpool vs Newcastle | 1.29 | 5.40 | 8.40 |
| 22:00 | 4956 | Twente vs SBV Excelsior | 1.28 | 5.63 | 8.44 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MORRISON AONGEZEWA DOZI, RASMI ZALAN FC KUCHEZA DAR

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amemwongezea programu maalumu winga wake, Bernard Morrison ili azidi kuimarika kwa ajili ya kujiandaa na michezo mbalimbali ya Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Septemba 6, mwaka huu Yanga watacheza dhidi ya Azam FC na Septemba 11, mwaka huu watawavaa Zalan FC ya Sudan, Kusini katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema hana presha na mechi hizo mbili dhidi ya Zalan kwa sababu kikosi chake kina nafasi nzuri ya kusonga mbele ukilinganisha na wapinzani wao.

Nabi alisema, wachezaji wake wana nguvu na wako tayari kwa kupambana dhidi ya wageni hao ambao wameomba kutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa kama nyumbani kwao.

Aliongeza, ana imani na kikosi chake lakini ameamua kumwongezea mazoezi Morrison ili afikie kiwango anachokihitaji kabla ya kuwavaa Zalan.

"Kulingana na ubora wa kikosi changu, nimeona nimpe Morrison (Bernard) mazoezi mengine tofauti ili kuwa imara zaidi na tayari kwa asilimia zote kwa sababu nina imani kubwa ya kufanya vizuri dhidi ya Zalan FC ili nitinge hatua inayofuata," alisema Nabi.

Aliongeza presha ya benchi lake la ufundi iko kwa Morrison ambaye kwa sasa anasimamiwa mazoezi na, Healmy Gueldich ambaye amemtengenezea programu maalum winga huyo.

"Tunahitaji kuwa na mawinga walio tayari kiushindani kabla ya kuingia katika hatua ya pili ya mtoano, tatizo Morrison bado hajawa katika kiwango bora ambacho tunakitaka, ndio maana tunamjenga zaidi," alisema Nabi.

Alisema, anatambua kama Morrison akiwa fiti kwa asilimia kubwa jinsi alivyo hatari, anaamini anaweza kuongeza kitu kwa kushirikiana na wengine wakiwako, Fiston Mayele na Stephan Aziz Ki.



Wachezaji wa Ihefu wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa Septemba 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro. **PICHA: MTANDAO**

# Refa Yanga, Coastal afungiwa

**Na Adam Fungamwango**

MWAMUZI, Rafael Ikambi aliyechezesha mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Coastal Union dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha amefungiwa kuchezesha ligi hiyo kwa mechi tatu huku mwamuzi msaidizi, Ferdinand Chacha na refa wa akiba, Abel William wakipewa onyo kali.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi baada ya kikao cha Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa ligi hiyo kilichokaa Agosti 26, mwaka huu kupitia mwenendo na matukio mbalimbali kimesema Ikambi kutoka Morogoro alishindwa kufanya uamuzi sahihi kwa mujibu wa sheria za mpira wa miguu kwenye tukio la mchezaji wa Coastal Union alimchezea rafu mchezaji wa Yanga, Yanick Bangala ambaye baada ya tukio hilo aliinuka na kwenda kumsukuma Albano.

Adhabu hiyo ni kwa uzingativu wa kanuni ya 42:1 (1.) ya Ligi Kuu kuhusu udhibiti wa waamuzi.

Katika taarifa hiyo, pia Bodi ya Ligi imeitozwa faini Sh. milioni moja kwa kosa la mashabiki wake kurusha chupa za maji uwanjani wakati wa mechi namba nne dhidi ya Polisi Tanzania kama ilivyoelezwa katika kanuni ya 47:1 ya Ligi Kuu kuhusu udhibiti wa klabu.

Pia Coastal Union, Kagera Sugar na Polisi Tanzania zimetozwa fainali ya Sh. milioni moja kila moja kutokana na makosa yanayohusiana na imani za kishirikina.

# Michezo

Jumatano Agosti 31, 2022
Nipashe



## Conte: Nataka Kane asaini mkataba mpya



Kocha Mkuu wa Yanga, Nassredine Nabi (katikati) akiwa na wachezaji wake, Stepane Aziz Ki (kulia), Djuma Shabani (kushoto) na Yanick Bangala baada ya kumaliza mazoezi kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC itakayochezwa Septemba 6, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAITOLEA MACHO AZAM FC

## •••Nabi aongeza dozi ya mazoezi kwa lengo la kuimarisha...

**Na Saada Akida**

ILI kuhakikisha timu yake inavuna pointi tatu muhimu, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, anatumia dakika 90, katika programu yake kuwapa wachezaji wake mazoezi mazito ya gym ufukweni kwa ajili ya kuimarisha stamina.

Kikosi hicho cha Yanga kilionekana kikifanya mazoezi hayo magumu juzi na jana asubuhi katika gym ya Gymkhana hapa jijini Dar es Salaam na jioni wakiendelea kujijenga kwenye viwanja vya Avic Town ambapo wameweka kambi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi, alisema amepanga kuwapeleka nyota wake katika ufukwe wa Coco ili kuendelea kuwanoa kwa sababu anahitaji wawe fiti na tayari kuwakabili Azam FC.

Nabi, alisema anataka kuona wachezaji wake wana pumzi ya kutosha na ndio programu maalumu aliyowaandalia nyota wake katika kipindi hiki cha mapumziko.

"Nahitaji kuwa na kikosi bora na chenye uwezo mkubwa wa kupambana katika dakika zote za mchezo, mazoezi ya viungo ni muhimu kwa sababu yanajenga utimamu wa mwili na kuwaweka imara kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mechi,".

"Napambana kujenga kikosi bora kwa sababu nahitaji kuwa na timu imara katika msimu huu ambao tumedhamiria kupambana kupata matokeo mazuri katika michezo yote tutakayocheza," alisema Nabi.

Kocha huyo aliongeza hataki kuona nyota wake 'wanakata' pumzi katikati ya mchezo na endapo hilo litatokea itawaweka kwenye wakati mgumu.

"Ninataka kikosi kiwe na uwezo wa kucheza katika kiwango cha juu, ndio maana tunapambana kuhakikisha wanakuwa imara na vile vile wana pumzi ya kutosha wakati wote, tunahitaji kuwa bora kuliko tulivyokuwa msimu uliopita," Nabi alisema.

Yanga inajiandaa kuvaana na Azam FC katika mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Septemba 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia saa 1.00 usiku.

Baada ya mchezo huo, Yanga itaendelea na maandalizi ya kuwavaa Zalan FC, kutoka Sudan Kusini katika mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa Septemba 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na marudiano yakifanyika katika uwanja huo huo.

Simba inayonolewa na Mserbia Zoran Maki, ndio vinara wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 wakifuatiwa na mabingwa watetezi Yanga, kila moja ikiwa na pointi sita mkononi.

## Simba, Al Hilal vita ya heshima

**Na Adam Fungamwango**

HATUPOI, hayo ni maneno ya nahodha wa zamani na Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola kuelekea mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya wenyeji, Al Hilal utakaochezwa leo kwenye mji wa Omdurman nchini Sudan.

Itakuwa ni mechi ya pili kwa vigogo hao wa Tanzania katika michuano maalum iliyoandaliwa na Al Hilal baada ya mechi ya kwanza iliyochezwa nchini humo dhidi ya Asante Kotoko ya Ghana ambapo ilishinda mabao 4-2.

Matola aliliambia gazeti hili wamejiandaa vizuri kuwakabili Al Hilal na wanaamini mechi hiyo itaendelea kuwasaidia wachezaji wake kujiimarisha kuelekea mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazofuata na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kocha huyo alisema benchi la ufundi linaendelea kufurahia fursa waliyopata ya kushiriki michuano ambayo inawapa nafasi baadhi ya wachezaji waliokosa maandalizi ya pamoja ya Pre Season ambapo waliweka kambi Misri na wengine waliokosa nafasi ya kucheza mechi mbili za awali za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Kocha (Zoran Maki) sasa ameanza kupata picha halisi ya mchezaji fulani yuko vipi na amtumie wapi, hii itatusaidia sana kwenye mechi za Ligi Kuu pamoja na Ligi ya Mabingwa Afrika kwa sababu wachezaji wanazidi kuimarika," alisema Matola.

Simba inacheza michuano hiyo bila ya nyota wake tisa walioko katika kikosi cha timu ya taifa (Taifa Stars), pamoja na Erasto Nyoni ambaye ni mgonjwa na Joash Onyango aliyeachwa hapa nchini.

Al Hilal, ilipata ushindi mnono katika mechi yake ya kwanza ambapo iliwatandika Asante Kotoko mabao 5-0.

Habari njema ni kwamba kiungo mkabaji, Sadio Kanoute, amejiunga na kikosi hicho akitokea kwao Mali alipokwenda kufuatilia suala ya hati za kusafiria.

Endapo Simba itashinda mechi hiyo ya leo, basi itakuwa bingwa wa michuano hiyo maalum, lakini ikitoka sare au kufungwa itakuwa imeshika nafasi ya pili nyuma ya wenyeji, Al Hilal.

Januari mwaka jana Simba iliwaalika Al Hilal na TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kushiriki michuano maalum iliyojulikana kwa jina la Simba Super Cup na wenyeji walitwaa ubingwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002